

KUCHAGULIWA NA KUSUDI

(MWALIMU)



BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

1. The first part of the paper is devoted to a discussion of the

main results of the paper.

2. The second part of the paper is devoted to a discussion of the

main results of the paper.

3. The third part of the paper is devoted to a discussion of the

main results of the paper.

“Mungu ndiye huwavuta watu kwake. Amefanya hivyo kupitia kwa Yesu Kristo. Hufanya kazi pia kupitia kwa watu. Kuwatumia watu wake kuwafikia wengine. Mungu anataka watu wote waokoke!”

Uliza: “Je! umempokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wako? Ikiwa bado unaweza kumpokea leo. Kristo alikufia wewe, na atakupa nguvu za kuishi kwa ajili yake.”

KUOMBA

1. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi wako wamwamini Yesu kama Mwokozi wao.
2. Waombee wanafunzi wako wawaonyeshe upendo watu ambao si Wakristo.

KUCHAGULIWA NA KUSUDI

(MWALIMU)

Kimeandikwa na Joshat M.M. Gikiri, Paul G. Karani, na
Rick M. Shisiali

BIBLE STUDIES FOR AFRICAN YOUTH

Africa Coordinated Curriculum
for Bible Study
Y2-2Ts

Used with permission of International Publications Services



Published by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

Printed by Nyanyambaga Printers
and Stationers
P. O. Box 8493 NAIROBI KENYA.

©Copyright, 1990
Baptist Publications House
All Rights Reserved

kufanya mpango mpya. Njia pekee ambayo angemfikia mwanadamu ni kwa kumtuma Mwanawe, Yesu Kristo.

“Manabii walizungumzia juu ya Mwokozi. Tazama Isaya 53. Unabii huu ulitimizwa wakati Yesu alipokuja. Alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu. Alisikitika na kuhuzunika. Alijitwika dhambi za ulimwengu wote. Hakujitetea wala kusema neno la lote alipohukumiwa. Aliteseka na kufa kwa ajili ya wanadamu wote. Haingefanyika hivyo bila upendo wa Mungu. Upendo wa Mungu ndio uliomfanya amtote Mwanawe pekee kuchukua mahali pa mwanadamu msalabani. Yesu ameleta wokovu kwa ye yote ambaye atampokea na kumwamini. Juhudi zake zote zinamwelekea kila mmoja.

“Waebrania 8:10 inasema, ‘...Nitawapa sheria zangu katika nia zao, Na katika mioyo yao nitaziandika....’ Mungu alitaka kila mmoja awe na wajibu wa wamuzi wake.”

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: “Neno agano, lina maana ya mapatano kati ya watu wawili au zaidi. Agano Jipya linatumia neno hili kuelezea uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Mungu ndiye aliyeanzisha kila kitu. Manabii wa Mungu walizungumzia kuhusu kuja kwa Mwokozi katika agano la kale. Unabii huu ulitimizwa wakati Yesu alipokuja.

“Yesu alibadili uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu. Aliwawezesha Wakristo kusema moja kwa moja na Mungu. Alikuwa daraja ya mwanadamu kumwendea Mungu.

“Waefeso 1:3-6 inasema kwamba Mungu alituchagua kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Mpango wa Mungu ulikuwa kumtuma Kristo afe ili wale watakaomwamini wapate uzima wa milele.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Uliza: “Je! agano ni nini?” (mapatano kati ya watu wawili au zaidi) “Je! kwa nini Mungu aliagana na wateule wake? Je! kwa nini aliagana upya nao?”

Uliza: “Je! Mungu aliamuaje kuagana upya nasi?”

Sema: “Mungu alitimiza ahadi yake alipomtuma mwanawe ulimwenguni. Yesu Kristo, Mwokozi, alikuja kama sehemu ya mpango wa Mungu wa kuwakomboa wanadamu. Dhambi, ilimtenganisha mwanadamu na Mungu, lakini hakutaka kupoteza viumbe vyake. Alipata wazo jipya la kuagana upya na mwanadamu.

“Yohana 3:16 inatuambia kwamba Mungu aliupenda ulimwengu sana, hata akaamua kumtuma Mwanawe ajitwike adhabu ya mwanadamu. Uamuzi mkuu wa mwanadamu ni kuchagua Mwokozi wake. Watu wengi hawajafanya uanuzi huu.”

MAELEZO

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waebrania 8:10. Uliza: “Je! ilimpasa Mungu aagane upya a Waisraeli? Je! ni nini kilichokuwa kimefanyika na agano la kwanza?”

Uliza: “Je! kwa nini aliweka sheria zake katika akili zao na kuliandika mioyoni mwao?”

Sema: “Mungu amekuwa akiagana na watu tangu mwanzo wa uumbaji. Aliagana na Ibrahimu, Nuhu, Musa na wengine wengi. Kusudi lake kuu lilikuwa kwamba Waisraeli wawe watu wake, na angewatumia kuyafikia mataifa mengine. Lakini walishindwa kumpokea na wakamkataa. Ilimpasa Mungu

YALIYOMO

SURA

UKURASA

1. Nchi Ya Ahadi.	5
2. Yusufu Aihama Nchi ya Ahadi.	10
3. Kuishi Misri.	14
4. Kutangatanga Nyikani.	18
5. Amri za Nchi ya Ahadi.	22
6. Kuitwaa Nchi ya Ahadi.	27
7. Kuishi kwa Haki Kanaani.	32
8. Kutenda Maovu Kanaani.	37
9. Mfalme Aliyechaguliwa na Wanadamu.	41
10. Mfalme Aliyechaguliwa na Mungu.	46
11. Masharti ya Mungu ya Kuishi Kanaani.	51
12. Kuangamizwa kwa Nchi ya Kanaani.	55
13. Mwokozi.	60

KUHUSU WAANDISHI

Josphat M. M. Gikiri ni mwalimu huko Muranga, Kenya. Ni mshiriki wa kanisa la Kaimiri.

Paul G. Karani ni mwalimu wa watu wazima na pia vijana wa huko Malindi, Kenya. Ni mshiriki wa kanisa la Ziyabomu.

Rick M. Shisiali, mtafsiri wa Baptist Publications House, Nairobi, ni mshiriki wa kanisa la Shauri Moyo.

kwanza. Agano hili jipya lingeunganisha Israeli iliyoanguka. Wanadamu wote wangemjua Mungu na kushiriki pamoja. Agano jipya lingeandikwa kwa mioyo na akili za wanadamu. Haingekuwa tu mpya, bali pia tofauti katika mkazo na kamilifu. Hawangemtii kwa sababu wanalazimishwa na sheria, lakini kwa sababu wanataka kumtii. Mungu aliahidi kuwasamehe na kusahau dhambi zao. Ushirikia huu mpya ungetokana na upendo wa Mungu.

Katika Agano la Kale mwanadamu alimtii Mungu kwa kutii sheria. Lakini sasa kila kitu kingetegemea neema na upendo wa Mungu. Uhusiano huu mpya ungezidisha ushirika wa mwanadamu na Mungu.

Isaya 53:2-5 inatupa mfano wa Mwokozi ambaye atatumwa na Mungu. Angekua kati yao. Hangukuwa na alama maalum ambazo mwanadamu angezitifuta. Angedharauliwa na kukataliwa. Angesikitika na kuhuzunika na kukasirika. Angekuwa mtumishi anayeteswa ambaye angemkomboa mwanadamu.

Tunasoma katika vifungu vya 6-12 kwamba angeteseka kwa ajili ya dhambi. Dhambi hii ni ya ulimwengu wote. Huwatenganisha na kuwatawanya watu kama kondoo. Lakini huu ni uamuzi wa mwanadamu mwenyewe. Kuteswa kwake kungesababisha kifo chake kama dhabihu ya dhambi za mwanadamu. Angeteseka ili kutimiza mpango wa Mungu. Watu wengi wangehesabiwa haki kupitia kwa mtumishi wa Mungu ambaye angejitwika mzigo wao. Watu waovu wangetenganishwa na watu wema.

Mwokozi angewaombea wale ambao wangempokea. Angechukua huzuni yao na kuadhibiwa badala yao.

SURA YA KUMI NA TATU
MWOKOZI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Waebrania 8:10; Yeremia 31:31; Isaya 53

VIFUNGU VYA LEO: Waebrania 8:10; Yeremia 31:31; Isaya 53

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Mungu anaweza kumwokoza na kumwongoza mtu ye yote.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Mungu alikuwa amesema kupitia kwa manabii kwamba atamtuma Mwokozi ambaye atawaokoa wanadamu kutoka dhambini. Angelipa deni ya dhambi za mwanadamu. Mwokozi angeleta haki na hukumu. Angeikomboa Israeli ndivyo Mungu angeanzisha ufalme wake duniani.

Mungu alijitayarisha kumtuma mwanawe, Yesu ulimwenguni. Angetumwa kwa wateule wa Mungu Israeli. Mungu alitaka kuwatumia Israeli kushiriki upendo wake na ulimwengu wote, lakini Israeli walikataa mpango wa Mungu. Walimkataa Mwokozi na wakaendelea kumtafuta Masihi.

Yeremia 31:31 inazungumzia kuhusu unabii wa Mungu kwamba ataagana upya na nyumba ya Israeli. Alipaswa kuagana upya kwa sababu walikuwa wamevunja agano la

SURA YA KWANZA
NCHI YA AHADI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Mwanzo 11:26-12:20

VIFUNGU VYA LEO: Mwanzo 12

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako” (Waebrania 11:8).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Mungu alimbariki Abram (Ibrahimu) kwa sababu alimtii.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Abramu aliishi maisha ya imani na utiifu. Alijulikana kama rafiki wa Mungu. Soma Yakobo 2:23. Kisha Mungu alibadilisha jina lake kutoka kwa Abram an kumwita Ibrahimu, yenye maana ya “baba wa mataifa.” Alikuwa wa ukoo wa Shem na mwana wa Tera. Babake Abram haliabudu Mungu. Aliitumikia miungu jinsi ilivyoandikwa katika Yohana 24:2. Abram ndiye aliyekuwa baba wa Waebrania na mataifa mengine.

Abramu alizaliwa Uru ya Wakaldayo ambako aliishi na baba yake, Tera, na ndugu zake, Nahori na Harani. Alimwoa Sarai. Harani alikufa kabla ya baba yake, na Tera akawachukua wanawe wakaenda mahali paitwapo Harani. Tera alifika huko, Harani.

Abramu alipofika umri wa miaka 75, aliitwa na Mungu, na akawaacha jamaa na baba yake. Mungu alimwambia aende

katika nchi atakayomwonyesha. Abramu hakujuu mahali nchi hiyo ilipo. Hakujuu cho chote kuhusu nchi hiyo, lakini alimwamini tu Mungu. Alikuwa tayari kufanya aliyooambiwa na Mungu.

Mungu alimchagua Abramu kama mwakilishi wake. Yeye ndiye angepokea na kuwaambia watu ujumbe wa Mungu. Alipoitwa aliondoka Harani pamoja na Lutu, mpwa wake, na wakaenda Kanaani wakipitia Shekemu na baadaye Betheli. Alimjengea Mungu madhabahu mahali hapa, na akaliitiza jina la Bwana.

Mungu alimwahidi Abramu kwamba atampa nchi yote ya Kanaani. Abramu alimdhahirisha Mungu imani yake na akamwabudu. Mungu alikuwa mwaminifu na akatimiza yote aliyomwahidi. Tutajifunza mengi jinsi aliyowatunza watu wake tunapojifunza masomo ya kitabu hiki. Ibrahimu (Mungu alibadalisha jina lake.) alikufa akiwa na miaka 175 na akazikwa kando ya Sara (Sarai) mkewe katika kaburi la Makpela ambalo alinunua kutoka kwa Efroni, mwana wa Sohari, Mhiti. Soma Mwanzo 25:7-10.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Mwalimu, anza somo hili kwa kusimulia hadithi hii: "Eliya alipata barua akiwa kijijini iliyomwita kwenda mjini kujifunza kazi aliyotamani sana. Hakuwa amewahi kwenda mjini. Alikuwa na wasiwasi jinsi ambavyo atafika shuleni bila kupotea. Mwishowe alikumbuka kuomba, na akamwambia Mungu amwongoze safarini."

Uliza: "Je! kwa nini watu huwa na wasiwasi au woga wanapoambiwa wafanye jambo ambalo hawajawahi kufanya?" Sikiliza majadiliano yao.

Mungu tunapofanya dhambi. Israeli walikuwa na sheria za Mungu ambazo wangufuata, lakini walianua kumwasi."

Uliza: "Je! ni nini kinachotusaidia kuwa waaminifu na kumtii Mungu?"

Sema: "Biblia inatufudisha jinsi ya kuishi mbele za Mungu. Hakuna kitabu kingine kilicho cha muhimu kama Biblia. Biblia ni chombo kinachotuonyesha makosa yaliyo maishani mwetu. Inatuonyesha njia ya kujirekebisha. Biblia ni ya muhimu kwetu kwa sababu inazungumzia shida zinazowakabili watu siku hizi. Tunaweza kuanza upya ushirika wetu na Mungu kwa kusoma Neno lake.

"Mungu atawahukumu wale wanaomwasi na kumkataa. Warumi 6:23 inasema, 'Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti....' Hii ndiyo adhabu ya Mungu kwa mtu afanyaye dhambi. Waovu wote watatenganishwa naye milele.

"Lakini mpango wa Mungu ni kwamba mwanadamu apate uzima wa milele. Yuko tayari kutusamehe dhambi zetu. Ni lazima tukiri dhambi zetu tumwombe msamaha na tumruhusu Mungu aumbe mfano wake ndani yetu.

"Wakristo ni wateule wa Mungu. Tunao wajibu wa kumpinga Shetani. Mungu ametupangia tuendeleze mpango na mapenzi yake ulimwenguni, lakini tunapaswa kwanza kumruhusu abadili maisha yetu."

KUOMBA

1. Waombee wanafunzi wako wawe na ushirika na Yesu ambao utawafanya waurithi ufalme wa Mungu.
2. Waombee waweze kumtumikia Mungu peke yake.

KUNDI 2: “Je! ni nini kilichosababisha kuadhibiwa kwa Yuda?” Kundi hili litapaswa kutoa mifano ya kuasi kwa Yuda. (2 Wafalme 24 na 25) “Je! ni nini kitakachotufanya sisi tuhukumiwe?” Wape muda wa kutoa mifano ya maovu.

Yaite makundi yote pamoja baada ya dakika kumi ili watoe ripoti yao. Jadili yale yanayopaswa kufanywa kuzuia kutokea kwa hukumu kama hiyo.

Sema: “Tunajua sasa sababu iliyoifanya Israeli iangamizwe. Hakuwa waaminifu mbele za Mungu. Mungu aliwaacha waangamizwe kama adhabu ya maovu yao.

Waulize wanafunzi watafute katika 2 Wafalme 24:3 sababu iliyowafanya Wababeli waivamie Yerusalemu. (dhambi za Manase)

Sema: “Ghadhabu ya Bwana ndiyo iliyoifanya Israeli iangamizwe. Aliacha washindwe na Wababeli.”

Wasaidie wanafunzi waelewe kwamba huu ulikuwa mwanzo wa hukukmu iliyoipata Israeli kwa sababu ya kumwasi Mungu. Waambie wanafunzi kadhaa wasome 2 Wafalme 24:17-20 kimoyomoyo kisha wajibu maswali haya:

1) Je! Sedekia alikuwa nani? (kifungu cha 17) 2) Je! alikuwa mtu wa aina gani? (kifungu cha 19) 3) Je! alifanya nini kilichoiletea Yerusalemu maangamizi? (vifungu vya 19-20)

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: “Waisraeli walimkasirisha Mungu kwa sababu ya uovu wao. Mungu aliudhika sana mpaka akawaondoa katika nchi yake. Walipelekwa uhamishoni.

“Mungu alitaka kushiriki na mwanadamu, lakini dhambi ilimtenganisha mwanadamu na Mungu. Huwa tunamwudhi

Sema “Abramu; katika somo letu la leo, anaweza kutufunza jinsi ya kutatua hofu zetu. Tafadhali fungua Mwanzo 12:1-9.”

MAELEZO

Sema: “Abramu aliitwa na Mungu kwenda katika nchi ambayo atamwonyesha. Abramu hakujua mahali nchi hiyo ilipo. Hakuwa ameonana na watu ambao wanaishi huko. Hata hakuwa na ramani ya kumwonyesha njia ya kwenda huko. Lakini Abramu aliondoka Harani kumfuata Mungu bila kusita. Alienda akiwa anamwamini Mungu.

“Mwanzo 12:3 inatuambia kwamba Mungu aliahidi kumbariki Abramu.” Mwambie wanafunzi mmoja asome vifungu vya 1-3.

Sema: “Mungu alisema kwamba atamtumia Abramu na kizazi chake kuwabariki watu wa ulimwengu wote.” Mwambie wanafunzi mwingine asome vifungu vya 4-9.

Sema: “Lutu alikuwa mpwa wa Abramu. Watu hawa wawili walikuwa na mali nyingi. Walipokuwa Harani, kwa hivyo walifanya kundi kubwa walipoanza safari yao. Walichukua kila kitu ambacho wangehitaji, hata mahema ya kuishi. Walikuwa na mifugo na watumwa wengi. Bwana alimtokea Abramu walipofika mahali paitwapo Shekemu. Naye akamwahidi.”

Uliza: “Je! alimwahidi nini?” (kifungu cha 7) “Je! Abramu alifanya nini?”

Sema: “Abramu alimjengea Mungu madhabahu hapo Shekemu alipomhakikishia kwamba atampa nchi hiyo. Alijenga madhabahu mengine alipofika Betheli na akaliitia jina la Bwana Betheli.

“Kulitokea njaa nchini wakati Abramu alipokuwa anaclekea Negebu. Alienda Misri kwa sababu mifugo wake walihitaji nyasi. Abramu alionyesha imani kuu na Mungu alikuwa

mwaminifu kumtimizia yote aliyomwahidi. Lakini tunaona katika Mwanzo 12:10-12 kwamba Abramam alishikwa na woga. Alimdanganya Farao kwa sababu ya woga wake." Mwambie mwanafunzi mmoja asome vifungu hivyo.

Endelea: "Tunajifunza katika sura inayofuata kwamba Abramam alirudi tena Betheli. Ni muhimu kwetu kukumbuka jambo hili kwa sababu hapo Betheli ndipo Abramam alikutana na Mungu mara ya mwisho."

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Mungu alimbariki Abramam kwa sababu ya imani na utii wake. Abramam alionyesha imani yake kwa kwenda katika nchi asiyojua. Alikuwa ameona miujiza ya Mungu na ahadi yake kuu, lakini aliogopa alipokaribia Misri.

"Je! huwa unaogopa kufanya jambo ambalo hulijui? Je! imewahi kutokea hivyo baada tu ya kuwa na wakati wa kumwamini Mungu na kumwona akifanya kazi maishani mwako? Huwa tunafurahia kitu ambacho tumekijua au kuwa nacho kwa muda mrefu. Huwa tunatarajia kuona jinsi kitakavyo kuwa.

"Mungu alimtarajia Abramam kuonyesha imani kuu. Alipaswa kumwamini Mungu kumtunza wakati ambapo hawezi kujitunza mwenyewe. Alipaswa kuenda mahali ambapo hapajui na imani kwamba Mungu atamshindia.

"Je! unaimani ya kumfuata Mungu po pote anapokuongoza? Imani ni karama ya Mungu. Ataikuza imani yako kama utamwomba.

"Mungu alimwita Abramam ili aache vyote alivyokuwa navyo. Alipaswa kuaacha jamaa yake, marafiki, desturi na mila na hali yake ya maisha. Hakujua yaliyo mbele yake. Mungu anawaita watu siku hizi waache maisha yao ya dhambi

Sedekia kama mfalme hakumtii Mungu. Alifanya maovu machoni pa Bwana Mungu. Alifanya yale yaliyofanywa na Yehoyakimu, na Mungu akamkasirikia sana. Mwishowe Mungu aliwaondoa machoni pake. Hakuwalinda tena kwa sababu walikuwa wamemwasi?

Baadaye Sedekia alimwasi mfalme wa Babeli. Jeshi la Babeli walikuja na kuharibu kila kitu kilichokuwa Yerusalemu. Waliwaua wana wa Sedekia mbele ya macho yake, wakachoma hekalu, makao yake na nyumba za watu. Kila kitu kiliharibiwa. Maovu yao ndio yaliyomfanya Mungu aache Israeli iangamizwe.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Sema: "Somo hili linatuambia kuhusu hukumu iliyowapata Israeli walipomwasi Mungu. Wafalme walifanywa watumwa wa Misri au Babeli. Israeli waliteseka sana mpaka wakatamani kuwa huru.

"Israeli waliirudia hali yao ya kuabudu miungu. Viongozi na watu waliamini kwamba Mungu hatawaangamiza kwa sababu walikuwa wateule wake. Walishindwa kuelewa adhabu ya dhambi zao na hukumu itakayofuatia. Walishindwa pia kuelewa adhabu ya kumwasi Mungu."

MAELEZO

Gawa wanafunzi wako katika makundi mawili na uwaambie wajibu maswali haya.

KUNDI 1: "Je! Yehoyakimu alifanya dhambi gani? (Waambie watafute jibu lake katika 2 Wafalme 23:37) Je! wafalme walioteuliwa wakati huu walikuwa na tabia gani?" Waambie wanafunzi waandike majibu yake ubaoni. "Je! kwa nini jeshi la Babeli lilivamia Yerusalemu?" (Soma 2 Wafalme 24:3.)

kuishi. Aliwapa kila kitu walichohitaji wakati walipoanza kuishi katika makao yao mapya. Lakini Israeli hawakumtii Mungu jinsi ilivyowapasa. Waliabudu miungu na kuishi katika dhambi. Mungu hangevumilia tena, kwa hivyo aliamua kuwakomesha wao na maovu yao.

Tunasoma katika 2 Wafalme 24:1-7 kwamba wafalme waliochaguliwa kutawala Israeli walimwasi Mungu. Yehoyakimu alianza kutawala akiwa na miaka 25. Alifanya maovu mbele za Mungu kama baba yake aliyemtangulia.

Yehoyakimu alikubali kumtumikia Mfalme Nebukadreza wa Babeli, lakini alimtumikia kwa miaka mitatu kisha akaacha. Mungu alikuwa amesema kupitia kwa manabii kuhusu adhabu ambayo wangepata. Alituma mataifa jirani kuangamiza Israeli na kuondoa machoni pake. Hangevumilia tena kuona maovu yao. Watu wasio na hatia waliteseka kwa sababu ya dhambi za Yehoyakimu.

Vifungu vya 10-14 vinatuambia kwamba Nebukadreza alituma jeshi lake kuvamia Yerusalemu. Aliwafuata mara tu walipokuwa wanaanza kushambulia. Mfalme Yekonia, mwana wa Yehoyakimu, alilazimishwa kujisalimisha kwa Wababeli. Alishikwa mateka pamoja na kila mtu aliyefanya kazi nyumbani kwake.

Hazina zote za nyumba ya Bwana na nyumba ya mfalme zilichukuliwa. Walikatakata vyombo vyote vya dhahabu ambavyo Sulemani alikuwa amevifanya jinsi manabii walivyotabiri. Watu na vitu vyenye thamani vilipelekwa Babeli. Watu masikini ndio walioachwa nyuma. Jeshi la Babeli walichoma hekalu na makao ya mfalme.

Vifungu vya 17-20 vinasema kwamba Nebukadreza, mfalme wa Babeli, alimtawaza Matania, mjomba wa Yekonia, kuwa mfalme mpya. Alibadilisha jina lake na kumwita Sedekia.

wanayofurahia na wamfuata kuanza maisha mapya. Ahadi zake ni kuu wale watakaomtii. Watakuwa na uzima wa milele mbinguni na watakuwa na uwepo wa Mungu maishani mwao mwote. Mungu ameahidi kuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wake. Haya yote yanategemea imani na utii wa kila mtu.

“Abramu aliporudi Betheli, alianza upya na kumwamini Mungu. Betheli palikuwa mahali ambapo Abramu alijenga madhabahu na kumwabudu Mungu. Alipaswa kumrudia tena Mungu na kupata maelezo ya hatua ya pili.

“Wakristo wanapaswa kumrudia Mungu kwa imani wanapoanguka. Ufunuo 2:5 inasema, “Basi kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza...” Je! unahitaji kumrudia Mungu?

“Biblia inafundisha katika Mithali 3:5-6, ‘Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako.’ Soma pia Zaburi 46:1-3.

KUOMBA

1. Waombee wanafunzi wako wamwamini Bwana na wamtumikie.
2. Omba kwamba watamruhusu Bwana kuyaongoza maisha yao.

SURA YA PILI
YUSUFU AIHAMA NCHI YA AHADI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Mwanzo 37 na 39

VIFUNGU VYA LEO: Mwanzo 37:12-14, 19-21, 26-28; 39:1-4

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Kila adhabu wakati wake haionekani kuwa kitu cha furaha, bali cha huzuni; lakini baadaye huwaletca wao waliozoezwa nayo matunda ua haki yenye amani” (Waebrania 12:11).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Mungu alimbariki Yusufu hata wakati wa shida.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Yakobo na wake zake wawili, Raheli na Lea, waliishi na mjomba (wa Yakobo), Labani, ambaye pia alikuwa baba ya wake zake. Yakobo alimpenda sana Raheli kuliko Lea kwa sababu alikuwa mzuri wa umbo. Hata hivyo, Raheli alikuwa tasa na mwenye huzuni nyingi. Alitamani sana kupata mtoto. Mwishowe Mungu alimfanya uzazi na akapata mimba. Alimzaa mtoto mwanaume na kumwita Yusufu, yenye maana ya “kuongeza” au “Mungu azidishe.” Soma Mwanzo 30:22-24.

Yusufu alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Raheli, lakini mwana wa kumi na moja wa Yakobo. Yakobo alimpenda sana. Alimshonea kanzu nzuri ndefu ambayo iliwafanya ndugu zake wamwonee wivu. Walimshitaki ndugu yake kwa Baba yao juu ya mambo anayofanya, ambayo pia yaliwakasirisha ndugu zake. Pia, Yusufu aliota ndoto ambazo zilielezea jinsi atakavyofanikiwa baadaye. Aliwaambia ndugu zake ndoto hiyo,

kwamba adhabu na mateso yanawangoja wale wanaoifanya mioyo yao kuwa migumu kuitikia mwito wa Mungu.

“Ushirika wetu na Mungu ni ghali sana. Ni lazima tujikane mambo fulani ili tumtumikie Mungu kwa mioyo yetu yote.”

KUOMBA

1. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi wako wawe waaminifu.

2. Mwombe Mungu akuonyeshe dhambi zako ili uweze kumwomba msamaha.

SURA YA KUMI NA MBILI

KUANGAMIZWA KWA NCHI YA KANAANI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: 2 Wafalme 24

VIFUNGU VYA LEO: 2 Wafalme 24

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “...Chagueni hivi leo mtakayemtumikia;...lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana” (Yoshua 24:15).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawaongoza wanafunzi wangu kutambua kwamba wale wanaomwasi Mungu wataadhibiwa kwa sababu ya dhambi zao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki, Biblia kwa kila mwanafunzi

MSINGI WA SOMO HILI

Mungu aliwapenda Israeli, wateule wake. Aliwatoa utumwani Misri. Aliwaongoza na kuwalinda katika vita. Aliwapa nchi ya

Sema: "Soma hili linatuonyesha umuhimu wa kutumia nafasi tuliyonayo kumtukuza Mungu badala ya kujitukuza sisi wenyewe.

"Mungu ametupa nafasi ya kutumika katika ufalme wake. Atatumia nafasi hii kama tu waaminifu na tutatii mapenzi yake. Ye yote anayekataa kumtii hupoteza nafasi hii ya kutumiwa na Mungu.

"Sisi tu na wajibu jinsi tunavyowatendea wengine. Mungu atawabariki tu wale ambao wanaoshiriki upendo wa rehema zake na jirani zao. Lakini atawaangamiza wale wanaowatesa wenzao.

"Mungu anataka ujitoe kwake kama Bwana na Mwokozi wako na uonyeshe wengine uwepo wake.

"Sulemani alimwomba Mungu hekima. Mungu alimpa hekima na akamwongezea utajiri, mali, baraka na maisha marefu ambayo hakumwomba. Mungu alilibariki taifa la Israeli kwa sababu walimtii na kuwa waaminifu.

"Mungu anafanya kazi maishani mwetu kutimiza kusudi lake wakati tunapomtii. Anataka tumruhusu atuongoze wakati tunapochagua mema na mabaya. Lakini wakati mwingi huwa tunashindwa na kusahau kutambua yale ambayo Mungu anafanya maishani mwetu.

"Tunapaswa kuchagua kati ya kumwamini Mungu na kuamini mambo ya dunia (elimu, mali, mamlaka). Mungu huwahukumu waovu na wenye dhambi.

"Ni lazima tumkubali Mungu kuwa Mungu wa pekee, na tumruhusu abadili maisha yetu kulingana na mapenzi yake. Ni lazima tutafute uongozi wa Mungu na tumwabudu kwa moyo wetu wote, roho na nguvu. Lakini tunapaswa tukumbuke

lakini ndugu zake walijaa wivu na hasira na wakamchukia sana.

Yusufu aliamini kwamba alipaswa kutofautishwa na wengine, hata jamaa yake. Alikuwa amechaguliwa na Mungu, na baba yake kuwa yule ambaye ataleta baraka. Mungu alikuwa amempangia baraka za ajabu ambazo angempa. Inasemekana kwamba Yusufu aliishi kati ya mwaka wa 1720-1570 kabla ya Kristo. Yusufu alikuwa babu wa makabila mawili, Manase na Efraimu.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Waambie wanafunzi wako wajiadiliane jambo hili: "Watu waliozaliwa katika jamaa moja hupendana sana wakiwa watoto. Lakini wanapoanza kuwa wakubwa wakati mwingi huanza kuoneana wivu hasa kwa yule anayefanya jambo maalum. Unaweza kuwa kwamba mmoja ni mwerevu kuliko wengine. Au mmoja ana kazi nzuri, au pesa nyingi kuliko mwingine. Je! unafikiri ni nini hasa huleta shida hizi?" Sikiliza majadiliano yao. Kisha umwambie mmoja wao asome Utangulizi kutoka vitabu vyao.

Sema: "Mungu ndiye hupeana uzama na kila mtu hubarikiwa kulingana na mpango wake. Tutajifunza leo kuhusu Yusufu, na tuone shida au matatizo yaliyompata."

MAELEZO

Sema: "Yusufu alitumwa na baba yake, Yakobo (ambaye anaitwa pia Israeli), kwenda Shekemu. Alimtuma awajulie hali ndugu zake, ambao walikuwa wakichunga mifugo ya baba yao. Walisafiri mwendo mrefu wakitafuta nyasi na maji. Yakobo alitaka kujua jinsi wanavyoendelea. Yusufu alipofika Shekemu,

alipata kuwa hawapo, wameenda Dothani, aliamua kwenda huko.

"Tunaanza kusoma katika Mwanzo 37:18 kwamba ndugu zake walimwona kwa mbali akija, na wakapanga kumwua. Mmoja wao alitaka kumwua, lakini Rubeni akaonelea wamtupe ndani ya kisima. Yeye alitaka arudi baadaye na amwokoe.

"Lakini walipokaa chini kula chakula, waliona msafara wa Waishmaeli wakija kutoka Gileadi. Yuda akawaambia wamwuze Yusufu kwa watu hao kama mtumwa. Waishmaeli walipofika Misri, walimwua Yusufu kwa Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari.

"Mwishowe ndugu zake walichinja mbuzi, wakapaka nguo zake damu na kwenda kumwonyesha baba yao. Alifikiri kwamba Yusufu amekufa." Soma Mwanzo 37:34.

"Mwanzo 39:1-4 inaonyesha kwamba Yusufu alikuwa mtumwa nyumbani kwa Potifa, akamfanya msimamizi wa nyumba yake na yote yaliyomo.

"Mwanzo 39 inatuambia pia majaribu yalikuja katika nyumba hiyo na Yusufu akafungwa gereza kwa kosa ambalo hakufanya. Hata hivyo katika hayo yote, Mungu alikuwa pamoja naye.

"Yusufu alipewa mamlaka zaidi na kuwa wa pili katika utawala wa nchi hiyo baada ya muda mfupi. Yeye ndiye aliyemfuatia mfalme."

Uliza: "Je! ni nani anayeweza kutuambia kilichofanyika baadaye?" (Kama hakuna aliye tayari kueleza, utapaswa kusoma aya ya mwisho ya sehemu ya Maelezo katika kitabu cha mwanafunzi, au usimulie hadithi kutoka Mwanzo 42-47.

"Petro alikasirika sana. Alimlaumu Gideoni kwamba anataka kuchukua kampuni yake. Alifikiri kwamba Gideoni anataka kazi yake. Alimwachisha Gideoni kazi mara moja.

"Gideoni alipotoka, alienda kuanzisha biashara yake mwenyewe ambayo ilikua kwa haraka sana. Lakini biashara ya Petro ilianza kuanguka."

Uliza: "Je! ni nini kilichokuwa kibaya ambacho Petro alimwazia Gideoni? Je! nini kingefanyika kama Petro angemruhusu Gideoni anunue hisa katika kampuni yake?" Wape muda wa kujibu.

Sema: "Tunaona leo yale yaliyowapata wafalme wa Israeli walikuwa waaminifu na wale ambao walikuwa waovu."

MAELEZO

Waambie wanafunzi wako wafungue Biblia zao katika 1 Wafalme 3. Waambie wafuate vifungu hivi wakati unapotumia Vifungu vya Leo kuelezea jinsi Mungu alivyowatuza wafalme waaminifu kama Sulemani. Waambie pia jinsi wafalme waovu walivyoiletea shida Israeli. Utapaswa kutumia maelezo yaliyoko kwenye Msingi wa Somo Hili na kutoka vitabu vya wanafunzi.

Uliza: "Je! Mungu alimfikiriaje Sulemani? Je! alimsaidiaje aendelee na kufanikiwa? Je! ni yapi yaliyowapata wafalme waovu? Je! mambo hayo yalilijumuje taifa la Israeli?" Jadilianeni pamoja. Andika ubaoni orodha ya baraka za Sulemani na adhabu aliyopewa Yeroboamu.

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Uliza: "Je! Mungu amewawekea masharti kwa watu wake ambao wanataka kumfurahisha? Hebu tufikirie juu ya masharti haya."

hekima na moyo wa kuwahukumu watu kwa haki (kifungu cha 9). Sulemani hakuomba utajiri, wala mali, wala heshima. Mungu alipendezwa sana na ombi la Sulemani. Mungu alikubali kutimiza ombi lake kwa sababu hakuomba mambo ya kujivunia. Lakini, Mungu aliahidi pia kumwongezea yale ambayo hakumwomba. Soma 1 Wafalme 3:13-14.

Wafalme wa kwanza 5:12 inatuambia kwamba Mungu alimpa Sulemani hekima. Aliishi kwa amani na jirani zake. Sulemani alianza kutafuta vifaa vya kumjengea Mungu hekalu. Taifa lake liliendelea sana wakati wa uongozi wake.

Tunapata mfano wa mfalme mwovu katika 1 Wafalme 14. Mfalme Yeroboamu alifanya maovu mbele za Mungu. Mungu alitumia Yeroboamu ujumbe kwa njia ya Ahiya, nabii wake. Alitumiwa ujumbe wa kuangamizwa kwa jamaa yake na taifa la Israeli. Nabii Ahiya alimwambia kwamba mwanawe angekufa na hataendelea kutawala mazishi maalum wanapokufa. Dhambi ya Yeroboamu ilimdhuru yeye mwenyewe, jamaa yake na taifa nzima. Aliwaongoza watu kuabudu sanamu, kwa hivyo walipaswa kulipia dhambi zao. Mungu hakuwalinda tena Israeli, bali aliwaacha wateseke.

Wafalme wengine wengi kama Rehoboam, Ahabu na Yoashi walimwasi Mungu pia. Walitumia mamlaka na ufalme wao kuliletea taifa lao shida na matatizo. Mungu aliwashitaka kwa kutotii amri zake.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Simulia hadithi hii: "Petro alifanikiwa katika biashara. Kufanikiwa kwake kulitokana na uaminifu wa Gideoni, mfanyakazi wake. Gideoni alimwendea Petro baada ya miaka mingi kupita na kumwambia kwamba angependa kununua hisa katika kampuni yake na awe na sehemu ya faida anayopata.

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Mungu huongoza hatua za kila mtu ambaye anamcha na kufuata mipango yake. Habadili kamwe."

Uliza: "Je! unafikiri utawatendeaje ndugu ambao watakutendea jinsi Yusufu alivyofanyiwa?" Wape muda wa kujadiliana. Watapaswa kusema pia jinsi Yusufu naye angefanya.

Uliza: "Je! Yusufu alifanyaje?"

Sema: "Yusufu aliwasamehe ndugu zake hata ingawa walimkosea. Hakuonyesha kuwa ana chuki au wivu moyoni mwake.

Uliza: "Je! ni rahisi kumsamehe mtu ambaye amekukosea?" Wape muda wa kujadiliana.

Sema "Yusufu aliwapenda na akawasamehe ndugu zake, na Mungu akambariki sana. Mwishowe aliweza baadaye kuwahudumia jamaa yake walipokuwa na hitaji kuu. Alilitimiza vizuri bila kulipiza kisasi.

"Kuna jambo lingine ambalo tunaweza kujifunza kutoka kwa somo hili. Yakobo alimpenda Yusufu. Jambo hili lilileta shida katika jamaa hii. Hata siku hizi shida hutokea wakati mtu mmoja anapopendwa kuliko wengine. Wakristo wanapaswa kuwapenda watu wote sawa kwa sababu wote wameumbwa kwa mfano wa Mungu. Wakristo wanapaswa kupendana ili ulimwengu ujue kwamba ni wanafunzi wa Kristo. Soma Yohana 13:34-35. Wakristo wanapaswa kusaidia watu wengine kwa sababu ya upendo wa Kristo."

KUOMBA

1. Omba kwamba upate nguvu za kuwasamehe wale wanaokukosea.

2. Omba kwamba wewe na wanafunzi wako mtawapenda na kuwaheshimu watu bila kufikiria maovu waliyokutendea.

SURA YA TATU KUISHI MISRI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Kutoka 1-7

VIFUNGU VYA LEO: Kutoka 5:1-8; 6:1; 12:29-41

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Naye Bwana, yeye ndiye atakayekutangulia, atakuwa pamoja nawe, hatakupungukia wala kukuacha; usiogope wala usifadhaika" (Kumbukumbu la Torati 31:8).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Mungu yu pamoja nao siku zote na hatawaacha kamwe.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Kila mwanafunzi atahitaji Biblia.

MSINGI WA SOMO HILI

Yusufu alikuwa kama makamu wa mfalme, na akawaleta jamaa yake waishi Misri. Walikuwa karibu watu sabini. Walikuja kuishi Misri kwa sababu kulikuwa na njaa kuu Kanaani, hali chakula kilikuwa Misri. Watu Waisraeli walikuwa wameongezeka na kuwa wengi. Yusufu, mwanawe Yakobo, na vizazi vyake waliongezeka sana wakiwa Misri.

Palitokea mfalme (Farao), baada ya Yusufu ndugu zake na kizazi chao kufa, ambaye hakumjua Yusufu na yote alivyofanya. (Kutoka 8:1) Mfalme huyo aliona kwamba wana wa Waisraeli wazidi kuongezeka. Walikuwa wenye nguvu na

SURA YA KUMI NA MOJA MASHARTI YA MUNGU YA KUISHI KANAANI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: 1 Wafalme 3:7-14; 5:12; 14:5-11

VIFUNGU VYA LEO: 1 Wafalme 3:7-14; 5:12; 14:5-11

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, Wala usizitegemee akili zako mwenyewe; Katika njia zako zote mkiri yeye, Naye atayanyosha mapito yako" (Mithali 3:5-6).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba watu huteseka wakati viongozi wao wanapokuwa waovu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki

MSINGI WA SOMO HILI

Israeli walikuwa sasa wanaishi katika Nchi ya Aahdi. Walikuwa wamefanikiwa na wanaishi kwa amani. Mungu aliwachagua wafalme waliotawala Israeli. Baadhi ya wafalme hao walikuwa waaminifu, hali wengine hawakuwa waaminifu. Shida iliwapata Waisraeli kwa sababu ya uovu wa wafalme wasio waaminifu.

Tunasoma katika 1 Wafalme 3:3-4 kuhusu Sulemani, mfalme aliyependa Mungu. Alienenda katika njia ya haki ya baba yake, Daudi. Sulemani alitafuta uongozi wa Mungu. Alimtolea Mungu sadaka za kuteketezwa.

Katika vifungu vya 5-9 Mungu alimtokezea Sulemani katika ndoto pale Gibeoni, mahali pa kuabudia. Mungu alimwuliza amwambie kile anachotaka ampe. Sulemani alimwomba

Sema: "Mungu hapendi uasi na uongo. Hawahurumii wale wanaotumia vyeo vyao kwa manufaa yao wenyewe. Anataka atutumie katika mpango wake ili tumtukuze.

"Mungu huwachaguwa watu hata leo. Anataka tufanye kazi anayotupa. Lakini tunapomwasi huchagua mtu mwingine badala yetu. Wakristo wote ni wa Mungu. Tumeitwa tuwe watumishi wa Kristo katika mambo yote tunayofanya.

"Roho Mtakatifu alibadili maisha ya Daudi. Ndivyo ilivyo hata sasa. Roho aliyeko ndani yetu huonyesha uwepo wa Kristo katika maisha yetu. Huu hututia nguvu. Sisi huanza kufanya mambo ambayo hatungeweza kufanya tunapoyatoa maisha yetu kwa Kristo. Sio sisi wenyewe tunaofanya hivyo: bali ni Kristo aishiye ndani yetu." Soma Wagalatia 2:20.

"Una kipawa ambacho Mungu anaweza kutumia. Unaweza kutumika katika ufalme wake. Unaweza kutumia vipawa hivyo na juhudi zako kumtumikia Kristo. Mungu anaweza kukutumia kuwafikia wengine jinsi alivyomtumia Daudi. Wewe umechaguliwa kufanya kazi maalumu katika mpango wako. Je! utamtii na kumruhusu abadili maisha yako?"

KUOMBA

1. Omba kwamba kila mwanafunzi atamwuliza Mungu amwongoze maishani mwake.
2. Waombee wanafunzi wako watii mwito wa Mungu.
3. Mwombee Mungu awajaze na Roho wake wanapokubali mwito wake wa kumtumikia.

walijaza nchi hiyo. Kwa hivyo alianza kuwaogopa, na akawafanya kuwa watumwa. Aliwapa kazi ngumu ya kufanya na kuwatendea maovu. Pia aliamua kuwaua watoto wanaume waliozaliwa na wanawake wa Kiebrania. Mpango huu ulileta shida kwa sababu wakungu wao walimcha Mungu, na hawakuwaua watoto hao. Soma Kutoka 1:15-22.

Lakini Bwana alikuwa na mpango wa kuwakomboa watu hao kutoka utumwani na kuwapeleka katika nchi aliyowaahidi. Soma Kutoka 3:7-8.

Mtoto Musa alizaliwa wakati watoto wachanga wa kiume walipokuwa wakitupwa katika mto Nile, lakini mama yake alipanga kumwoko. Mwishowe alilelewa katika makao ya mfalme kama mtoto wa binti ya Farao. Musa alipotimiza miaka arobaini, Mungu alimwita kuwaongoza wana wa Israeli kutoka utumwani. Musa alitoa sababu nyingi sana za kutotaka kwenda Misri kwa sababu alifikiria hawezi kazi hiyo, lakini Mungu aliahidi kuwa pamoja naye.

Sura kumi na mbili za kwanza za kitabu cha Kutoka zinazungumzia kuhusu jinsi Mungu alivyowatayarisha na kuwatoa watu wake nchini Misri. Mwalimu, leo utwaacha wanafunzi wako wakusaidie kufundisha kwa kutafuta majibu ya maswali ya leo.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Anza somo hili kwa kusema: "Kuna watu wengi ulimwenguni ambao hawana uhuru. Hawawezi kujiamulia mambo wanayotaka. Wengine hawawezi kuwa na mali yao binafsi wala kuchagua kazi watakayofanya. Hawawezi kumwabudu Mungu jinsi wanavyotaka."

Uliza: "Je! kwa nini hufanyika hivyo?" Wape muda wa kujadiliana.

Uliza: "Je! ni nini kinachoweza kufanywa?" (Hakikisha wanafunzi wanaelewa kwamba wanapaswa kuwaomba watu hawa wenye mahitaji.)

Sema: "Wana wa Israeli, wateule wa Mungu, walikuwa na hitaji kuu. Waliishi utumwani nchini Misri, na wale waliowasimamia waliwahangaisha sana. Lakini wakati wa Mungu ulipofika, alimwita Musa kuwaongoza Waisraeli kutoka utumwani na kuwapeleka katika Nchi ya Ahadi.

"Utabarikiwa sana kama utasoma hadithi yote kutoka sura za kwanza kumi na tano za kitabu cha Kutoka. Pengine utanza kusoma katika wakati wako wa kimya na Mungu kila asubuhi."

MAELEZO

Sema: "Musa alitoa sababu nyingi wakati Mungu alipomwita. Alifikiri kwamba hawezi kufanya yale aliyoambiwa na Mungu, lakini Mungu aliahidi kuwa pamoja naye. Fungua kitabu cha Kutoka 4:1-10 kuona sababu alizotoa Musa na yale ambayo Mungu alimwambia." Waambie wanafunzi waseme kwa maneno yao wenyewe.

Sema: "Ujasiri wa Musa ulikua alipoanza kazi yake na kuona kwamba Mungu yuko pamoja naye. Ndugu yake, Haruni, alikuwa msaidizi na mnenaji wake jinsi Mungu alivyoahidi. Walimwendea Farao na kumwambia yale Mungu aliyosema."

Uliza: "Je! wana wa Israeli walifikiri nini juu ya jambo hili?" (Kutoka 5:21)

Uliza: "Musa alimrudia Mungu na kumwambia shida hii, na Mungu akatoa ahadi nyingi katika Kutoka 6:1, 6-8. Je! alimwahidi nini?"

Samweli alimlilia Sauli. Yeye ndiye aliyemtia mafuta kuwa mfalme. Walikuwa pamoja kwa muda mrefu. Ndipo Samweli akalilia kuanguka kwake.

"Mungu alimwambia Samweli aache kumlilia Sauli. Alikuwa amemkataa. Hakufaa kuwa mfalme. Mungu alimwambia Samweli aende nyumbani kwa Yese na amtie mafuta mwanawe mmoja kama mfalme mpya. Mungu alikuwa amewachagulia watu mfalme."

Uliza: "Je! Samweli alijua mtoto yupi wa Yese ambaye angemtia mafuta?" (Jibu linapatikana katika 1 Samweli 16:6-13.)

Sema: "Mungu alikwisha kutayarisha kila kitu. Alitaka tu kumtumia Samweli kuthibitisha uchaguo wake. Alijua moyo wa Daudi. Alikuwa na tabia za kiongozi, hasa mfalme Daudi hakujua mpango wa Mungu kwa maisha yake, lakini alikuwa tayari kufuata mwongozo wa Mungu. Alikubali wajibu wake mpya bila kulalamika.

"Mungu alipendezwa na Daudi. Alimbariki na akamjaza na roho wake. Hakumwacha awe peke yake. Alimwongoza tangu siku hiyo."

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Uliza: "Je! kwa nini Sauli alichaguliwa na mwishowe akakataliwa? Sauli hakutumia vizuri wajibu wake. Alitumia eheo chake kujitukuza mwenyewe badala ya kumtukuza Mungu. Alishindwa kutii na kutimiza mpango wa Mungu."

Uliza: "Je! nini hufanyika wakati Wakristo wanaposhindwa kumtii Mungu? Je! huwa wanaonyesha picha gani kwa waamini au wapotevu? Je! Mungu huwaadhibu?" Wape muda wa kujibu.

Uchaguo wa Mungu ulibadili maisha ya Daudi. Mfalme atakayetawala alisimama mbele ya Samweli. Samweli alimpaka Daudi mafuta mbele ya jamaa yake.

Kifungu cha 13 kinasema, "...na roho ya Bwana ikamjilia Daudi kwa nguvu tangu siku ile...."

Roho wa Bwana alidhihirisha kwamba Daudi amekubaliwa na Mungu. Sasa alikuwa tayari kuwa mtumishi wa Bwana. Bwana alimwongoza Daudi tangu siku hiyo. Uchaguo wa Mungu ulikuwa mwema kwa watu wake.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Utangulizi katika kitabu chake kama wote hawajasoma.

Uliza: "Je! kwa nini Paulo alifikiri kwamba hawezi kufanya yale aliyoambiwa na Mchungaji? Je! kulifanyika nini alipojaribu kufanya hivyo?"

Sema: "Wakati mwingi woga hutufanya tumzuie Mungu asitutumie. Huwa tunafikiri kwamba hatuwezi kufanya jambo hilo hata kabla ya kulijaribu. Tazama 1 Samweli 16. Daudi hakujua kwamba anaweza kuwa mfalme. Lakini Mungu alimwonyesha wazi alipokubali wajibu huo. Alimruhusu Mungu ambadilishe na kumtayarisha kwa kazi hiyo kuu. Daudi hangeweza kutambua uwezo na vipawa vyake kama angekataa kupakwa mafuta. Lakini alikubali bila kulalamika."

Uliza: "Je! huwa unaulalamikia ujumbe wa Mungu kabla ya kumpokea na kutenda jinsi unavyosema?"

MAELEZO

Sema: "Sauli alikuwa mfalme wa Israeli, lakini alishindwa katika kazi yake. Alimkataa Mungu naye Mungu akamkataa.

Sema: "Waisraeli waliendelea kupata shida, na Farao akakataa kuwaruhusu waondoke. Mwishowe Mungu aliwaleta Wamisri misiba ya huzuni. Soma Kutoka 7-11, na useme baadhi ya misiba hiyo."

Uliza: "Je! ni nini kilichomfanya Farao kuwaruhusu Waisraeli waondoke?" (Kutoka 12)

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Mungu ni waajabu mwenye huruma na wa haki. Hasahau kamwe watu wake. Hasahau kamwe ahadi zake kwao.

"Mungu aliahidi kuwakomboa watu wote kutoka kwa utumwa wa Shetani, na alifanya hivyo kupitia kwa Mwanawe, Yesu Kristo. Tafadhali fungueni Wakolosai 1:13-14." Mwambie mmoja wao asome vifungu hivi.

Sema: "Mungu alimchagua Musa, akamlinda na akamtayarisha kufanya kazi yake. Mungu amekuchagua kufanya kazi maalum, na atakulinda na kukutayarisha kufanya kazi hiyo. Soma Wafilipi 1:6." Mmoja wao asome kifungu hiki.

Sema: "Watu hukosa kuwa na subira katika shida zao. Hawako tayari kungojea Mungu awafundishe jambo ambalo wanapaswa kujua. Ndivyo ilivyokuwa kwa Wamisri na ndivyo ilivyo hata sasa. Mungu anatufundisha kwamba atakuwa pamoja nasi kwa yote tunayofanya. Ni lazima tujifunze kumwamini na kungojea kutimia kwa wakati wake. Fungua Isaya 40:31. Je! nani atatusomea kifungu hiki?"

Sema: "Mungu yu pamoja nasi siku zote. Hututangulia mbele na kututayarishia njia. Hatatuacha kamwe. Atusaidie ili tuwe na moyo wa kumsubiri."

KUOMBA

1. Omba kwamba wewe na wanafunzi wako mtakuwa tayari kumsubiri Bwana.
2. Jitoe kwake akutumie jinsi anavyotaka. Waombee wanafunzi wako pia wafanye hivyo.

SURA YA NNE

KUTANGATANGA NYIKANI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Kutoka 16:2-3; 17:2; Hesabu 13:1-3, 17-20, 25-14:2, 11

VIFUNGU VYA LEO: Kutoka 16:2-3; 17:2; Hesabu 13:1-3, 17-20, 25-14:2,11

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Wenye haki watairithi nchi, Nao watakaa humo milele" (Zaburi 37:2a).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba ni lazima wadumu katika kumwamini Mungu ili wafurahie baraka zake.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Njoo darasani na ramani ya nchi yo yo yote inayoonyesha njia.

MSINGI WA SOMO HILI

Mungu alimwahidi Ibrahimu, baba wa taifa la Waebrania, kwamba yeye na jamaa (kizazi) yake watarithi nchi ya Kanaani. Tazama Mwanzo 13:15. Watu walienda Misri walipoondoka Kanaani kwa sababu ya njaa. Walifanywa watumwa wa Farao, lakini Mungu aliwakomboa kutoka katika utumwa huo. Alimtumia Musa kama kiongozi wao.

Sauli. Mungu hakutaka Israeli ianguke, kwa hivyo alipanga kumchagua mfalme mpya. Mungu alimwambia Samweli aijaze mafuta pembe yake na aende Bethlehem, nyumbani kwa Yese.

Kupaka mafuta kulikuwa ishara kwamba kitu au mtu anawekwa wakfu kwa kazi maalum. Mafarao wa Misri walitiwa mafuta. Makuhani na manabii wa Israeli walitiwa mafuta.

Mungu alimwambia Samweli mahali pa kwenda na mtu wa kuona. Samweli hakujua ni yupi kati ya wana wa Yese ambaye angemia mafuta, lakini Mungu aliahidi kumwonyesha. Samweli aliogopa kwamba Sauli atamwua ikiwa atajua kazi anayoenda kufanya. Lakini Mungu alimwambia achukue ndama na aende kutoa sadaka huko Bethlehem, kisha amwalike Yese na wanawe kuhudhuria. Samweli alimtii Mungu. Mungu alimwezesha Samweli kujua la kufanya.

Tunasoma katika kifungu cha 7 kwamba wana wa Yese walipita mbele ya Samweli wakati huo wa kutoa sadaka. Samweli alipomwona Eliabu, mzaliwa wa kwanza, alifikiri kwamba ndiye aliyechaguliwa. Eliabu alikuwa mnene, mwenye nguvu na sura ya kupendeza. Lakini Mungu alimwambia Samweli kwamba siye aliyemchagua. Mungu alijua moyo wake. Alimkumbusha Samweli kwamba "...Bwana haangalii kama binadamu aangaliavyoo..." (kifungu cha 7). Bwana huutazama moyo bali si sura ya nje.

Samweli wa kwanza 16:10-13 inasema kwamba wana wa Yese saba walipita mbele ya Samweli, lakini Bwana hakuwachagua. Samweli alimwuliza Yese kama anao watoto wengine. Yese alimwambia kwamba mdogo wao yuko, lakini anachunga kondoo. Samweli alimwambia Yese awatume watu wamlete. Kijana mwenye macho mazuri na umbo la kupendeza aitwaye Daudi alifika. Mungu akasema kwamba ndiye aliyemchagua.

2. Omba kwamba watategemea uongozi wa Mungu maishani mwao.

3. Mwombe Mungu akusaidie kuwa mfano mwema kwa wanafunzi wako.

SURA YA KUMI

MFALME ALIYECHAGULIWA NA MUNGU

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: 1 Samweli 16; 18; 21; 23

VIFUNGU VYA LEO: 1 Samweli 16:1, 7, 10-13

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Nawe mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote” (Kumbukumbu la Torati 6:5).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawahimiza wanafunzi wangu wamruhusu Mungu awachagulie mambo wanayotaka.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Mungu alimkubali Sauli kama mfalme wa kwanza wa Israeli. Alikuwa pamoja naye, na akamlinda alipotawala Israeli. Lakini Sauli alianza kuacha njia ya Mungu. Alimwasi Mungu, na akafuata njia zake mwenyewe. Mwishowe Mungu alimkataa kama mfalme, na akachagua mfalme mwingine. Alijua kwamba kulikuwa na mtu mwaminifu katika nyumba ya Yese. Yeye ndiye aliyechaguliwa na Mungu kama mfalme.

Samweli ndiye aliyemweka Sauli wakfu na akampenda kwa sababu ni mfalme. Pia, alikuwa na wasi wasi juu ya ufalme wa Israeli. Mambo haya yalimhuzunisha Samweli. Katika 1 Samweli 16:1, Mungu alimwambia Samweli aache kumlilia

Watu walielekea Kanaani walipotoka Misri. Walikuwa watu wapatao elfu mia sita. Nguzo la wingu liliwaongoza wakati wa mchana, na usiku waliongozwa na nguzo ya moto ili wapate kusafiri mchana na usiku. (Kutoka 13:21-22)

Walienda hadi Bahari ya Shamu na kupiga kambi hapo. Waliona milima upande wa kulia na kushoto na bahari ilikuwa mbele yao. Farao aliufanya moyo wake kuwa mgumu, na akaamua kuwafuata Waisraeli. Waisraeli waliogopa sana walipoona wanafuatwa na askari wa Farao. Walimlalamikia Mungu na Musa, lakini Mungu akaahidi kuwafanyia maajabu. Soma Kutoka 14:10-31, jinsi walivyovuka Bahari ya Shamu.

Shida za Israeli hazikuisha hata baada ya mwujiza huu. Soma Kutoka 33. Walishindwa kumwamini Mungu kabisa.

Watu walitambua kwamba wamekosa kitu kimoja ambacho walikuwa nacho nchini Misri. Hapakuwa na maji walipofika jangwani. Ilipofika siku ya nne, waliyafikia maji ya Mara, lakini yalikuwa machungu. Walimlalamikia Musa, na Mungu akamwonyesha mti. Musa akaitupa fimbo katika maji hayo nayo yakawa matamu ya kunywa. (Kutoka 15:22-25)

Hatimaye walifika katika bara ya Sini, na wakakosa chakula. Watu walinungunika tena, na Mungu akawapa mkate wa mana kila asubuhi na nyama ya ndege kila jioni. Hadithi hii ya kisisimua inapatikana katika Kutoka 16.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Utangulizi kutoka katika kitabu chao.

Sema: “Tunaelewa sababu iliyomfanya Thomasi kutafuta njia mwituni, lakini Je! kwa nini wana wa Israeli walikuwa wakitangatanga nyikani?” Wape muda wa kukumbuka baadhi

ya sura mlizojifunza ili wajue kwamba Waisraeli hawakuwa wamemwamini Mungu. Walilalamika na kunungunika kila wakati walipopatwa na shida. Walikuwa wameona miujiza ya Mungu kwao, na walikuwa na ahadi za Mungu, lakini hawakuonekana kama wanamwamini.

MAELEZO

Sema: "Mungu aliwapa watu wake kila kitu walichohitaji, lakini wao walilalamika na kumshuku. Aliwaongoza kutoka Misri na kuvuka Bahari ya Shamu. Aliwapa maji na kuyafanya kuwa matamu ili wayanwe. Mungu aliwapa mkate na nyama walipohitaji chakula. Tunaona katika Kutoka 17:1-6 kwamba watu walihitaji tena maji, na Mungu akawapa maji kutoka kwa mwamba." Soma vifungu hivi.

Sema: "Hata hivyo watu hawakuamini uongozi na ulinzi wa Mungu, ndipo wakatangatanga nyikani. Safari yao ingekuwa fupi sana, lakini walimaliza miaka arobaini na hawakuwa wameingia Nchi ya Ahadi.

"Mwishowe walipiga kambi katika nyika ya Parani. Bwana alimwambia Musa awatume watu waende kupeleleza nchi ya Kanaani." Waambie wanafunzi wafungue Hesabu 13.

Endelea: "Mungu alimwambia Musa awatume watu kumi na wawili, mmoja kutoka katika kila kabila ili waone jinsi nchi hiyo ilivyo. Musa awapa maagizo ya kufuata, na akawaambia walete baadhi ya matunda ya nchi hiyo ili watu wote wayaone." Mwambie mwanafunzi mmoja asome Hesabu 13:17-20. Kisha waseme ripoti ambayo wapelelezi hao walileta.

Sema: "Wapelelezi walirudi baada ya siku arobaini, na wote wakakubali kwamba nchi hiyo imejaa maziwa na asali. Walileta matunda waliyopata huko na yalikuwa mazuri sana. Lakini walisema kwamba watu wa huko ni majitu makubwa. Miji yao

"Wakati mwingine Wakristo husisitiza kufanya kinyume cha mapenzi ya Mungu. Mungu huwaacha wafanye jinsi wanavyotaka. Lakini ni lazima wateseke kwa uamuzi wao mbaya. Tunawezaje kuepuka jambo hili? Tunapaswa kutafuta mapenzi ya Mungu kwa yote tunayofanya. Sisi ni watoto wake. Ametupa uzima na ni lazima atutumie kwa kumtumikia. Ni lazima tumwishie yeye. Hakuna jambo lililo dogo kwetu ambalo hatuwezi kumpelekea. Hakuna pia lililo kubwa kwake ambalo hawezi."

Sema: "Hatupaswi kuamua kulingana na tamaa zetu. Hatupaswi kuamua ili tuwapendeze rafiki zetu. Tunapaswa kufanya uamuzi ambao Bwana atakubali na pia utampendeza. Mungu atatubariki tukimfuata yeye na njia zake.

"Watu walikataa kusikiliza maonyo ya Samweli kuhusu mfalme. Wakristo wanapaswa kuwa wepesi wa kusikia maonyo ya Mungu. Hatupaswi kufanya mambo kwa sababu watu wengine wanafanya. Ni lazima tuige mfano wa Kristo, tutembe kama yeye na tuishi kama yeye. Tukifanya hivyo tutakuwa tunamshuhudia Kristo.

"Tunapaswa kumwomba Mungu atuongoze. Anaweza kumtuma mtu wa kutusaidia. Pengine anaweza kutumia Neno lake, Biblia. Anaweza kutujibu tunapomba. Mungu anaweza kutumia njia nyingi kutuonyesha mapenzi yake.

"Mungu anapaswa kutawala uamuzi wetu. Amekuchagua na kusudi. Unapaswa kuamua kumwacha afanye mapenzi yake maishani mwako."

KUOMBA

1. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi wako watafute mapenzi yake maishani mwao.

Walikuwa watu wa Mungu, lakini walishindwa kutafuta ushauri wake. Waliamua wao wenyewe na kufuata njia zao wenyewe. Mungu aliwaacha wafanye jinsi walivyotaka.”

MAELEZO

Mwalimu, tumia maelezo ya Msingi wa Somo Hili kueleza jinsi wazee walivyomwendea Samweli na ombi lao la mfalme. Waambie sababu zilizowafanya kutaka mfalme. Mwambie mwanafunzi mmoja asome 1 Samweli 8:5.

Sema: “Israeli walitaka mfalme. Hawakumfikiria Mungu kama Mfalme wao wa mbinguni. Waliamini kwamba mfalme wa kidunia ndiye atakuwa mwema zaidi. Walitaka wawe kama mataifa mengine!”

Uliza: “Je! Samweli alifikiri nini aliposikia ombi la wazee hao? Je! Samweli alimwomba nani msaada?” (Mungu)

Uliza: “Je! Bwana alimwambia nini Samweli? Je! watu walikuwa wakimkataa nani?” Wape muda wa kujibu kila swali. Ongezea maelezo ambayo wamesahau.

Sema: “Mungu alikuwa amewafanyia Waisraeli mambo makuu, lakini, walifikiri kwamba mfalme wa kidunia angewafaa zaidi. Mungu hakukataa ombi lao, bali alimwambia Samweli awatafutie mfalme. Maisha hayangewaendea vizuri. Wangeteseka na kupoteza mali zao, wana na binti zao.” Soma kifungu cha 19.

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: “Wakristo wengi humkataa Mungu jinsi Waisraeli walivyomkana. Je! watu humkataaje Mungu siku hizi? (kwa kukataa kumpokea, kwa kufuata njia zao wenyewe, kwa kukosa kumshuhudia au kutosoma Biblia na kuomba)

ilikuwa imejengwa maboma. Kumi kati yao walisema kwamba hawawezi kuitwaa nchi hiyo.

“Lakini kulikuwepo na wapelelezi wawili, Yoshua na Kalebu. Watu hawa walikumbuka ahadi za Mungu. Walikumbuka kwamba Mungu alikuwa amewafanyia maajabu, na waliamini kwamba atawawezesha kutwaa nchi hiyo. Walijaribu kuwashawishi watu, lakini hawakuweza kamwe.

“Mungu aliamua kwamba wateule wake hawataingia nchi ya Ahadi kwa sababu ya kutomwamini. Walipaswa kurudi tena nyikani. Wale waliokuwa bado watoto ndiyo wanguweza kuingia baadaye, baada ya wazazi wao kufia jangwani. Wale wapelelezi wawili waliokuwa na imani wangukubaliwa kuingia Nchi ya Ahadi na kuwaongoza watoto baada ya wazazi wao kufa.”

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: “Ni rahisi kwetu kuona makosa ya wana wa Israeli. Mungu alikuwa amewabariki sana, lakini hawakumwamini.”

Uliza: “Je, ni rahisi sisi kuona dhambi zetu?” (Usingojee majibu.)

Sema: “Tumeona mara nyingi baraka za Mungu kwetu. Ametutimizia mahitaji yetu, lakini wakati sisi hulalamika na kumshuku badala ya kumwamini. Hata tuna baraka zaidi ambazo Waisraeli hawakuwa nazo. Tunayo Biblia ambayo inatuonyesha jinsi Mungu alivyowatimizia watu wake tangu zamani. Tuna ahadi zake kwamba habadiliki kamwe, kwa hivyo atatutimizia nasi pia.

“Yoshua na Kalebu ndio wapelelezi pekee waliotoa ripoti ya haki kuhusu Kanaani. Hawakupinga kwamba watu hao ni majitu. Walikubali kwamba miji imezungukwa na maboma, lakini walijua kwamba Mungu atawaongoza kuitwaa nchi hiyo.

“Wale wengine kumi walitoa ripoti ambayo haikuwa na ujasiri. Waliwafanya watu wawe dhaifu na kutomwamini Mungu. Watu waliteseka kwa sababu ya ripoti yao na hawakuishi kamwe katika Nchi ya Ahadi.”

Uliza: “Je! unataka kuwapa watu wengine ujasiri au hofu?”
(Usingojee majibu.)

Sema: “Unaweza kuwatia watu ujasiri kwa imani yako. Mwombee Mungu akusaidie uwe baraka kwa watu wengine ambao wanayaangalia maisha yako. Mwombe aikuze imani yako.”

KUOMBA

1. Mshukuru Mungu kwa kupata nafsi ya kufundisha somo hili, na umwombe akusaidie kuwatia moyo wanafunzi wako wawe na imani kuu.
2. Omba kwamba utakuwa mwaminifu mbele za Mungu na watu wengine.

SURA YA TANO

AMRI ZA NCHI YA AHADI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Kutoka 20

VIFUNGU VYA LEO: KUTOKA 20:1-25

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Usiwe na miungu mingine ila mimi” (Kutoka 20:3).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba amri za Mungu ziliandikwa kuwasaidia watu wamtii.

kumtegemea Mungu tu. Alikuwa Mungu wao! Samweli aliona pia kwamba wanamkataa yeye na kazi yake. Samweli alimwambia Mungu ombi la wazee hao, na Mungu akamwambia awafanyie jinsi wanavyotaka. Alimwelezea wazi yule wanayemkataa. Haikuwa Samweli, walikuwa wakimkataa Mungu. Walimkana Mungu, mfalme wao. Lakini Mungu alimwambia Samweli awaonye kuhusu mahitaji ya mfalme. Soma 1 Samweli 8:11-18 kuona mahitaji ya mfalme ambaye watu walitaka awatawale.

Kifungu cha 19 kinatuambia kwamba wakati Samweli alipowaambia watu juu ya mahitaji ya mfalme, wao walikataa kumsikiliza. Walitaka kuwa na mfalme iwapo atakuwa mwema au mbaya. Walimwelewa vizuri Samweli, lakini hawangeweza kukubaliana naye. Walitaka mfalme na walikuwa tayari kuishi kwa uamuzi wao.

Bwana alimwambia Samweli awatimizie watu hitaji lao. Watu walirudi nyumbani baada ya Samweli kuwahakikishia kwamba atawapa mfalme.

KULIFUDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Uliza: “Je! huwa ni rahisi kwako kutafuta mashauri ya wenzako kabla ya kufanya jambo lo lote? Sema baadhi ya mambo ambayo utataka ushauri kabla ya kufanya?” Wape muda wa kujadiliana. Ikiwa wameshindwa la kusema unaweza kuanza kwa kusema kujenga nyumba, kuunganisha waya za umeme, ugonjwa n.k.

Uliza: “Je! utamwendea nani akushauri?”

Sema: “Wakati mwingine Wakristo husahau kutafuta ushauri wanapopanga mambo yao. Wakati mwingine huwa hawafuati mashauri wanayopewa. Waisraeli walifanya vivyo hivyo.

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi wangu wajifunze kufuata yale ambayo Mungu amewachagulia maishani mwao.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Tuliona katika Sura ya Nane jinsi Waisraeli waliacha kumfuata Mungu. Walianza kufuata tamaa zao wenyewe na kukata mashauri yao wenyewe.

Samweli alikuwa sasa mzee sana. Aliwafanya wanawe wawili kuwa waamuzi wa Israeli, lakini walianza kufanya maovu. Walipokea rushwa na hawakutenda haki. Soma 1 Samweli 8:1-3.

Vifungu vya 4-5 vinatuambia jinsi wazee wa Israeli walivyomwendea Samweli na hitaji. Wazee hawa ni wale walioakilisha Israeli. Walitaka mabadiliko. Walitoa sababu mbili za ombi lao, umri wa Samweli na uovu wa watoto wake Samweli. Aliheshimiwa sana, lakini wanawe hawakuheshimiwa. Walikuwa kinyume cha baba yao. Walikuwa wachoyo na walipokea rushwa na walitoa uamuzi kwa kupendelea. Wazee wa Israeli hawakuwaamini wana wa Samweli kama waamuzi.

Wakamwambia Samweli, "...Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote" (kifungu cha 5).

Watu walitaka mfalme! Je! kwa nini? Walisema kwamba wana wa Samweli hawaenendi katika njia zake, walitaka mtu ambaye angetoa uamuzi wa haki kati yao na kuwaongoza katika vita. Walifikiri kwamba mfalme atafanya taifa lao kuwa lenye nguvu.

Soma vifungu vya 6-9. Samweli hakutaka Israeli wawe na mfalme. Alifikiri kwamba wanamkataa Mungu. Walipaswa

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki au karatasi kubwa na kalamu

MSINGI WA SOMO HILI

Kutoka ni kitabu mojawapo cha amri. Unapojifunza somo hili utagundua kwamba Mungu aliwasaidia watu wake na neno lililoandikwa ili wajue hasa maana ya kumtii. Mungu alipaswa kuwaandikia watu wake. Alikuwa ameona jinsi walivyomwasi na akaanza kuwaambia maana ya kutii.

Kitabu cha Kutoka kiliandikwa na Musa. Kutoka ina maana ya kuondoka. Kinazungumzia kuhusu wana wa Israeli wakijitayarisha kuingia Nchi ya Ahadi kutoka Misri. Musa alikuwa kiongozi wao.

Tunasoma pia katika kitabu hiki jinsi Mungu alivyomwita Musa, shida zilizowapata wana wa Mungu na jinsi Mungu aliyyowaongoza kutoka utumwani. Waliendelea kufanya dhambi, na Mungu alijua kwamba ni lazima awape amri. Amri hii haingewazuia kufanya dhambi, lakini ingewasaidia kujua yale wanayastahili kufanya au kutofanya. Mungu aliwapa watu wake Amri Kumi.

Kutoka 19 inaonyesha yale ambayo watu walipaswa kufanya ili kupewa amri hizo. Mungu mwenyewe ndiye aliyenena sheria hizo. Hii inaonyesha mamlaka ya sheria hizi na hutusaidia kujua kwamba zimepewa watu wote. Ni mwongozo wa kuufikia utakatifu. Mungu hufurahii watu wanaomkosea kwa kuvunja sheria zake.

Mungu alitoa kwanza amri nne zinazoonyesha jinsi mtu anavyopaswa kushirikiana naye. Amri za mwisho sita zinaonyesha jinsi watu wanavyopaswa kushirikiane wao kwa wao.

Tutajifunza sheria za Mungu leo na tuone yale anayotarajia tufanye. Mkristo anapaswa kutii amri za Mungu. Mtu anapokuwa Mkristo, hupokea Roho Mtakatifu. Roho humsaidia kumtii Mungu. Roho Mtakatifu humsaidia kutambua kwamba Mungu yupo na kuimarisha imani ya Mkristo huyo.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Uliza: "Je! wana wa Israeli walipewa amri zipi kwenye Mlima Sinai?" Andika maneno "Amri Kumi" ubaoni au kwenye karatasi.

Uliza: "Je! Waisraeli walikuwa wapi kufikia mwisho wa sura ya nne ya vitabu vyenu?" Wanaweza kuangalia katika somo la nne kama wameshindwa kujibu.

Uliza: "Je! Mungu alipendewa na wateule wake?" (La. Aliudhika sana kwa sababu hawakumwamini.)

Sema: "Hebu tuone yale ambayo Mungu alifanya kufuatia dhambi ya watu wake."

MAELEZO

Sema: "Mungu aliwaona watu wake wakiwa wanajitenga naye. Walikuwa wakimtendea dhambi na pia walitendeanwa wao kwa wao. Waliishi kulingana na tamaa zao badala ya mapenzi ya Mungu. Mungu alijua kwamba ni lazima awape sheria zilizoandikwa.

"Mungu alimwita mtumishi wake, Musa na akamwambia awakusanye watu pamoja kwenye Mlima Sinai. Mungu alimwambia Musa na Haruni waupande mlima huo, lakini watu hawakukubaliwa kwenda pamoja nao. Wao walibaki chini

"Mungu anataka tumwonyeshe kwamba tunampenda kwa kutii amri zake. Hataki tufanye mambo kwa uchoyo au tamaa, bali kwa uvumilivu. Tunapaswa kuwafikiria wenzetu kuwa bora kuliko sisi wenyewe.

"Maisha ya Mkristo si rahisi. Kuna majaribu ya kila aina, lakini Yesu atawasaidia wale wanaomtengemea. Tutafanikiwa kama tutampa Yesu nafasi ya kwanza maishani mwetu."

KUOMBA

1. Omba kwamba utaukubali uongozi wa Mungu maishani mwako.
2. Mwombe Mungu akujaze na Roho wake na akuongoze katika ukweli wote.
3. Mwombe Mungu akuonyeshe vipawa vyako ili uweze kumtumikia vizuri.

SURA YA TISA

MFALME ALIYECHAGULIWA NA WANADAMU

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: 1 Samweli 8-9

VIFUNGU VYA LEO: 1 Samweli 8:1-10, 19-22

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi zao, na kuiponya nchi yao" (2 Mambo ya Nyakati 7:14).

kulipiza kisasi kwa maovu waliyomtendea. Mungu alimwepusha kila mara, lakini yeye hakumshukuru Mungu kwa kumsaidia. Alifikiri kwamba Mungu ataendelea kumsaidia hata akitenda maovu kwa sababu yeye ni Mwisraeli.

“Hakufanikiwa kwa yote aliyofanya, kwa sababu alimpuuza Mungu. Alifikiri kwamba tamaa zake zafaa kuliko mpango na njia za Mungu.”

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: “Amri za Mungu zingemfanya Samsoni kuwa baraka kuu kwa watu wake, lakini aliamua kutenda dhambi. Dhambi huzuia ushuhuda wetu kama Wakristo. Sote tu wenye dhambi, lakini Mungu ametuletea msamaha na mwanzo mpya ikiwa tutamwomba Mungu atatutumia tunapochagua kumfuata.”

Uliza: “Je! Samsoni angefanikiwa bila ya kusaidiwa na Mungu? Je! Wakristo wanaweza kufanikiwa bila Mungu?”

Sema: “Mungu anajua jina la kila mmoja. Anajua mawazo na matendo yetu. Anajua kama tunamfuata kwa moyo wa kweli. Mungu anataka kututumia kufanya kazi aliyotupatia. Anataka tuwaambie wapotevu habari zake. Tukimfuata, tutafanya hivyo.”

Uliza: “Je! tunapaswa kumfuata nani kama Wakristo? Je! ni lazima tufanye nini?”

Sema: “Luka 9:23 inajibu swali hili. Ni lazima tujikane nafsi zetu na tumfuate Yesu kila siku, sio tu mara moja kwa wiki. Hivyo basi tutakuwa katika maisha yetu ya Kikristo.

“Mwana riadha hawezi kutuzwa asiposhindana kulingana na sheria zilizowekwa. Ndivyo ilivyo na Wakristo. Mungu hawezi kukutuzi na kukubariki usipomfuata kwa moyo wa kweli. Mpende Mungu, na umtii, naye atakutuzi uzima wa milele.

ya mlima huo. Walisikia sauti ya Mungu, lakini hawakuweza kumwona.

“Mungu alisema amri zake na akaziandika kwenye mbao za mawe ili kuwapa watu wake amri hizi. Zingewaonyesha watu jinsi Mungu anavyotaka waishi. Wangejua yale wanayopaswa kufanya kumfurahisha Mungu. Hebu tu some pamoja amri hizo katika Kutoka 20:1-17.” Wanafunzi kadhaa wasome vifungu hivi.

Sema: “Utaona kwamba amri za kwanza nne zinamwambia mwanadamu jinsi kumtendea Mungu. Jambo la kwanza tunalojifunza ni kwamba Mungu ni mkuu. Mwanadamu hapaswi kamwe kuwa na miungu mingine.”

Uliza: “Je! watu huabudu miungu mingine ipi maishani mwao?” (Wape muda wa kujibu. Pengine watasema pesa, kazi, elimu, mali au jamaa.)

Sema: “Mungu anasema kwamba vitu hivi havipaswi kuwa muhimu zaidi kuliko yeye maishani mwetu. Pili, Mungu alikataza wanadamu kutengeneza sanamu na kuziabudu. Sanamu hazipaswi kuabudiwa. Ni dhambi kufanya hivi.

“Tatu, Mungu alisema watu wanapaswa humheshimu jina lake. Hapaswi kulitaja bure jina la Bwana ila kama ni kwa ibada ya kweli.

“Hatimaye, Mungu aliwaambia watu jinsi ya kuitumia siku ya sabato. Sisi huikumbuka siku hii wakati wa Jumapili. Ni siku ambayo ni tofauti sana na siku zingine zote wa wiki. Ni siku ya kuabudu na kupumzika.

“Amri sita za mwisho zinamwambia mwanadamu wajibu wake kwa wengine. Mungu anataka kila mtu atii amri zake. Amri ya kwanza kati ya hizi inazungumzia kuhusu wajibu wa mtu kwa wazazi wake. Amri hii ina ahadi. Je! ahadi hiyo ni ipi?”

(kwamba siku zako ziwe nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako)

Sema: “Amri inayofuatia inamkataza mwanadamu kuua. Yesu alisema jambo fulani kuhusu kifungu hiki. Tafadhali tufungue Mathayo 5:21-22. Je! ni nani atatusomea vifungu hivi?” Ngojewa wasome na mjadiliane.

Sema: “Amri inayofuata inazungumzia juu ya uzinzi. Hebu tuone yale ambayo Yesu alisema kuhusu uzinzi. Tazama Mathayo 5:27-28.” Mwambie mwanafunzi mmoja asome.

Sema: “Amri inayofuata inakataza wizi. Tunajua kwamba kuingia nyumbani mwa mtu na kuchukua mali yake ni wizi. Pia tunajua kwamba kuchukua kalamu ambayo si yako ni wizi. Je! Mungu anaweza kuacha hayo yatendeke kama kwamba haoni?

“Amri nyingine inazungumzia juu ya kudanganya. Mungu hapendi uongo. Anawatarajia watoto wake waseme ukweli. Soma Waefeso 6:14. Hakuna nafasi ya uongo katika maisha ya Mkristo.

“Mwishowe, hatupaswi kutamani kitu cha mtu mwingine. Ni lazima tufurahi kwamba wanacho, nasi tufurahie tulicho nacho.”

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Uliza: “Je! ni rahisi kuvunja amri za Mungu?”

Uliza: “Tunawezaje kujilinda kwa kutovunja amri za Mungu?” Wape muda wa kujadiliana. Waongoze wanafunzi wako kuona kwamba ni lazima wamtii Mungu kwa kushika amri zake na kuwa waaminifu. Wanapaswa kusoma Neno la Mungu kujua yale ambayo Mungu anataka wafanye.

Sema: “Mkristo ana baraka maalum katika Roho Mtakatifu. Huja kuishi ndani ya Mkristo ye yote anayempokea Yesu

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Uliza: “Je! Anna aliyeko katika hadithi ya Utangulizi alifuata maagizo aliyopenda ya kupika chakula? Je! kwa nini hakufuata hali alijifunza jinsi ya kuyatumia? Je! nini kilichofanyika?”

Uliza: “Je! ni rahisi kwako kufuata mashauri ya wazazi au waalimu wako? Je! kwa nini?” Andia majibu yao ubaoni.

Sema: “Vivyo hivyo hatuwezi kumfuata Mungu kwa nguvu zetu wenyewe. Samsoni alimkubali Mungu, lakini hakumruhusu aongoze maisha yake. Alipatwa na shida iliyomzuia kufanya kazi ya Mungu. Hebu sasa tujifunze habari zake.”

MAELEZO

Sema: “Samsoni angemfanyia Mungu mambo makuu kama hangechagua kufuata tamaa zake mwenyewe. Mungu alipanga kuzaliwa kwake, na akasema Samsoni atakuwa Mnaziri. Lakini Samsoni alifikiri kwamba tamaa zake zafaa kuliko njia ya Mungu.

“Waamuzi 14 inatuambia kwamba Samsoni alimpenda mwanamke, Mfilisti. Aliwaendea wazazi wake na kuwaambia kwamba wamletee mwanamke huyo awe mkewe. Walishangaa sana. Kulikuwa na wanawake wengi wa Kiebrania ambao Samsoni angeweza kuoa, lakini alijichagulia bila ya kumwomba Mungu.”

Uliza: “Je! kulifanya nini wakati Samsoni alipoenda nyumbani kwa mkewe? Je! kwa nini arusi ilivunjika?” Mwambie mwanafunzi mmoja asome Waamuzi 15:1-2.

Sema: “Tunaambiwa katika vifungu vya 9-19 kwamba kulikuwepo vita kati ya Samsoni na Wafilisti. Wafilisti walifikiri kwamba wanapigania haki yao. Samsoni naye alitaka

Mungu alikuwa ameonya juu ya watu wasio Waebrania. Hawakumwabudu Yahwe, Mungu wa kweli. Waliabudu sanamu. Maisha yao yangewavutia Waisraeli. Lakini Samsoni hakutii maneno ya Mungu. Alimpuza! Akamwambia baba na mama yake, "...Nimemwona mwanamke huko Timna,...basi mnapatie nimwoe" (Waamuzi 14:2).

Mungu hakumpangia hivyo Samsoni. Ilikuwa tamaa yake kuunganishwa na mtu asiye mwamini. Hakufanikiwa na arusi hiyo. Mwishowe hakumwoa! Mungu alijua moyo wa Samsoni, lakini alikuwa tayari kumtumia. Hata hivyo, dhambi za Samsoni zilimfanya Mungu asimtumie vilivyo. Hata hakufikiria kutubu!

Waamuzi 15:1-8 inatuambaia jinsi Samsoni alipata habari kwamba mkewe alikuwa amepewa rafiki yake. Samsoni hakumwambia Mungu shida hii. Alitenda jinsi alivyofikiria. Alishika mbweha mia tatu akawafunga wawili wawili, akawasha moto na kuuweka katikati ya mikia yao. Aliwaachilia wakaingia katika mashamba ya Wafilisti na kuchoma ngano nyingi sana. Wafilisti walikasarika na wakapanga kulipiza, kisasi. Walimchoma mkewe, baba yake na mali yao yote. Samsoni aliwaua Wafilisti wengi alipopata habari hii. Mwisho akaenda kukaa katika ufo wa jabali la Etamu.

Wafilisti walimfuata wakiwa na nia ya kumshika, lakini Samsoni alijazwa na Roho wa Bwana. Aliwaua Wafilisti elfu kwa taya ya punda. Mungu alimwokoza asife kwa kumpa maji. Soma Waamuzi 15:9-19.

Huwa tunapata taabu tunapompuuza Mungu maishani mwetu. Samsoni, mtu wa Mungu na Mnaziri, alijifikiria kwanza badala ya Mungu. Alifuata tamaa zake mwenyewe na hakumruhusu Mungu amwongoze. Alishindwa kuwakomboa Waisraeli kutoka kwa adui zao.

kama Mwokozi. Roho Mtakatifu hukaa ndani ya kila mwamini na husaidia kujua mema na mabaya. Ni msaidizi na mshauri ambaye hatakuacha kamwe. Mungu alimleta Roho Mtakatifu atusaidie kumtii. Je! utamkumbali leo na umwombe akusaidie uishi kwa kutii amri za Mungu?"

KUOMBA

1. Mwombee kila mwanafunzi aelewe kwamba amri za Mungu zinatuhusu hata sisi.
2. Omba kwamba wasio Wakristo watampokea Yesu kuwa Mwokozi wao wakati wa somo hili.
3. Omba kwamba Neno la Mungu litaenezwa ulimwenguni mwote.

SURA YA SITA

KUITWAA NCHI YA AHADI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Yoshua 5:1, 6-7, 10; 6:1-20

VIFUNGU VYA LEO: Yoshua 5:1, 6-7, 10; 6:1-20

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "...Lakini yeye anayenitumaini ataimiliki nchi, na kuurithi mlima wangu mtakatifu" (Isaya 57:13b).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawasaidia wanafunzi kujifunza kwamba wanapaswa kumtii Mungu ili waweze kushinda maishani.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Kitabu cha Yoshua kinatuambia jinsi Yoshua alipigana na kuishinda Kanaani, Nchi ya Ahadi. Waisraeli walikuwa wamekaa nyikani kwa miaka arobaini ili watu waliomwasi Mungu wafe. Kizazi hiki hakikuamini ahadi za Mungu. Mungu alitaka kizazi kipya warithi nchi aliyowaahidi babu zao. (Yoshua 5:6-7).

Yoshua 5:1: Waisraeli walikuwa wamefika Yordani na kupiga kambi Gilgal, mashariki mwa mpaka wa Yeriko. Wafalme wote wa Waamori na Wakanaani waliwaogopa sana Waisraeli. Walikuwa wamesikia jinsi Mungu alivyoyatenganisha maji ya Mto Yordani ili wavuke. Walijua kwamba hawawezi kamwe kupigana na Bwana Mungu.

Waisraeli walipaswa kufanya mambo mawili ya kujitayarisha kuitwa nchi hiyo. Mungu alimwamuru Musa awatahiri wanaume wote wa Kiyahudi. Hawakuwa wametahiriwa kwa sababu walitumia muda mwingi kutangatanga nyikani. Pili, walikula sikukuu ya Pasaka ili kukumbuka jinsi Mungu alivyowakomboa kutoka utumwani Misri.

Je! kwa nini walipaswa kufanya mambo hayo? Mungu alitaka wajitayarishe kiroho. Walipaswa kujua kwamba Mungu ndiye aliyekuwa nguvu zao.

Waisraeli walikuwa sasa watu wa Mungu. Mungu aliwaahidi ushindi ikiwa watamtii na kuwa waaminifu.

Yoshua 6:1-7 inasema kwamba mji wa Yeriko ulifungwa kutoka ndani na kutoka nje kwa sababu ya Waisraeli. Ulikuwa ngome ya Wakanaani, lakini Waisraeli walipaswa kuushinda kabla ya kuendelea mbele.

Bwana alimwahidi Yoshua ushindi. Alimwambia kwamba amekwisha wapa Yeriko na wenyeji wake. Mungu alimwambia

SURA YA NANE

KUTENDA MAOVU KANAANI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: Waamuzi 13-16

VIFUNGU VYA LEO: Waamuzi 15; 16:1

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: “Ee Mungu, uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu” (Zaburi 51:10).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba kumwasi Mungu huleta adhabu.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Ubao na chaki

MSINGI WA SOMO HILI

Kuzaliwa kwa Samsoni kulikuwa kwa ajabu. Mungu alimwondolea mkewe Manoa utasa, na akamzaa mtoto mwamume, Samsoni. Alikusudiwa kuwa Mnaziri. Alitolewa kwa Mungu kwa sababu maisha yake yangekuwa tofauti sana. Hakupaswa kukata nywele zake, kunywa divai au kugusa mzoga wa wote. Alipaswa kuishi maisha ya haki mbele za Mungu. Alipaswa kumfuata Mungu na kumtumikia. Bwana alimbariki na akajazwa na Roho wa Bwana. Soma Waamuzi 13.

Lakini Samsoni alianza kumsahau Bwana alipoanza kukua. Alianza kutenda kinyume cha Mnaziri. Aliishi kulingana na tamaa zake mwenyewe. Tunaona katika Waamuzi 14 kwamba moyo wa Samsoni ulijaa upendo wa kidunia. Alienda Timna, mji wa Wafilisti na akampenda mwanamke wa Kifilisti. Je! jambo hili lilikuwa zuri kwake kama Mnaziri au kama Mwisraeli?

Mungu anapaswa kumtii. Hatuwezi kutii tu sehemu ya amri za Mungu. Tunapaswa kutii zote!

“Wakristo wanamhitaji Mungu. Tunahitaji uwepo na uongozi wake maishani mwetu. Tunapaswa kumwabudu kila siku. Atatupa nguvu na hekima ya kumfuata.

“Mkristo anapaswa kujifunza kuyashinda majaribu kwa maombi, kusoma Biblia, kushiriki na waamini wengine na kushuhudia. Tunapaswa kuwa jinsi Mungu anavyotaka tuwe. Wokovu katika Yesu ndio unapaswa kuwa wa thamani kwetu.”

Uliza: “Je! Warumi 12:1 inatuambia tufanye nini?” Mwambie mwanafunzi mmoja asome kifungu hiki.

Sema: “Kuwa mwenye haki si jambo la wakati mmoja tu. Ni jambo la kufanya kila siku. Tunapaswa kumwabudu Mungu kila siku maishani mwetu. Hivyo basi tutaishi katika ushirika naye. Kisha Mungu atatutuzi kwa uaminifu wetu.

KUOMBA

1. Mwombe Mungu akusaidie wewe na wanafunzi wako mwabudu kwa Roho na kweli.

2. Waombee wanafunzi wako wajitoe kwa Mungu kama dhabihu iliyo hai. Omba kwamba watakuwa tayari kumtii Mungu.

Yoshua jinsi ya kuuteka mji huo. Alimpa maarifa ya vita ambayo hayakuwa ya kawaida. Walipaswa kuuzunguka mji huo wakipiga tarumbeta! Mungu alikuwa tayari kuwaonyesha Waisraeli nguvu zake.

Tunaona katika vifungu vya 8-16 kwamba Yoshua aliwamuru Waisraeli kufanya yote waliyoambiwa na Bwana. Aliwachukua makuhani saba, tarumbeta saba na sanduku la agano. Aliwachukua watu wenye silaha na walinzi, na wakaanza kuuzunguka mji wa Yeriko mara moja kila siku. Siku ya saba waliamka asubuhi na mapema, na wakauzunguka mji huo mara saba. Makuhani walipiga tarumbeta zao kwa sauti kuu mara ya saba, na Yoshua akawaambia watu, “...Pigeni kelele; kwa maana Bwana amewapeni mji huu” (Yoshua 6:16). Maangamizi yalifuata kelele zao.

Kuta za mji huo zilianguka chini! Waisraeli waliingia katika mji huo na kuangamiza kila kitu kwa upanga. Hakuna kitu kilichobakia ila Rahabu, yule kahaba, ambaye aliwaficha wajumbe walioenda kupeleleza mji wa Yeriko. Waisraeli walichukua fedha, dhahabu na vyombo vya shaba, na chuma na kuvipeleka “...katika hazina ya Bwana” (kifungu cha 19). Vitu hivi vilikuwa vitakatifu na vya dhamani mbele za Mungu.

Kifungu cha 20 kinasema kwamba kelele ziliufanya ukuta ule uanguke. Waisraeli walienda na kuutwaa mji huo. Mungu aliwashindia Israeli. Alitimiza ahadi yake na akawasaidia kuitwaa nchi hiyo.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Uliza: “Je! Mungu aliwaonyeshaje Waisraeli nguvu zake walipoufikia Mto Yordani? Je! jambo hili liliwaambukizaje wafalme wa Kanaani?” Wape muda wa kujadiliana. Wasaidie waeleze kilichofanyika.

Uliza: "Je! inamaanisha nini kutii amri za Mungu? Je! Mungu ametupa amri zipi?" Wape muda wa kujibu.

Mwambie mwanafunzi mmoja asimulie au aisome hadithi ya Utangulizi kutoka katika vitabu vyao.

Uliza: "Je! Yakobo na Yohana waliwezaje kushinda mashindano ya mbio?" Watapaswa kusema walifuata maagizo ya mwalimu wao. Walijitayarisha mapema ili kuwa tayari wakati wa mashindano. Pia walikuwa na moyo wa kushinda.

Sema: "Tutajifunza leo jinsi Waisraeli walivyoshinda baada ya kutii amri za Mungu. Walifuata maagizo ya Mungu, na akawawezesha kufanikiwa. Hebu sasa tufungue kitabu cha Yoshua."

MAELEZO

Sema: "Mungu alimtumia Yoshua kuwaongoza Waisraeli kuitwaa Kanaani. Walipaswa kumtii na kumwamini Mungu ndipo washinde.

"Mungu alikuwa amewatia Wakanaani hofu. Je! ilikuaje hivyo?" (Yoshua 5:1) Waulize wanafunzi kama wanaweza kuogopa kupigana na adui ambao Mungu amewaongoza kuvuka mto bila kuyakanyaga maji.

"Waisraeli walipaswa kujitayarishia kazi hii maalum. Alimwambia Yoshua awatahiri waume wote wa Kiebrania. Hawakuwa wametahiriwa kwa sababu waliishi miaka mingi nyikani wakitangatanga. Pia walikula Pasaka. Je kwa nini?" (Watu walipaswa kujitayarisha kiroho ili kupata nguvu na uongozi wa Mungu.) "Mwishowe walikuwa watu wa Mungu baada ya kujitoa kwake.

"Mungu alijaribu imani na utii wa watu wake kwa kuwapa mtindo wa ajabu wa kupigana vita. Alitaka kuona kama Waisraeli walimtengemea yeye. Ilikuwa wazi kwamba wataitwa

Sema: "Samweli aliwaambia watu wakutane Mispa na kuwaongoza kwa maombi ya kukiri na toba. Walifunga na wakamwaga maji mbele za Bwana. Hii ilionyesha dhambi zao na hitaji lao la kutaka kusamehewa."

Uliza: "Je! Mungu alikubalije haki yao?" (vifungu vya 10-11)

Sema: "Walimpendeza Mungu. Aliwalinda na kuwawezesha kushinda adui zao. Aliwapa amani na akawabariki Mungu alikuwa Mwaminifu kwao. Waisraeli walimjengea Mungu madhabahu pale Gilgal na Betheli. Walitaka wawe na mahali pa kukutania na kumtolea Bwana sadaka. Walitaka kumwabudu Mungu na kumtii kama Bwana wao."

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Israelili ilikuwa taifa la Mungu, lakini walianza kuabudu miungu ya nchi walioikalia. Mungu alimtumia Samweli kuwasaidia wamrudie Bwana."

Uliza: "Je! Wakristo huabudu miungu ipi siku hizi?" Wape muda wa kujibu. Wanaweza kusema pesa, mali, magari, elimu, heshima n.k.

Sema: "Tunaweza kusema kwamba Mungu ni Mungu wetu, hali tunaadubu vitu vingine. Ni lazima tuchague kati ya kumwabudu Mungu na vitu vingine. Mungu huwaadhibu wanadamu wanapofanya dhambi. Lakini pia huwabariki wanapomtii. Mungu hutuongoza katika maombi na ibada. Yuko pamoja nasi na hutuongoza katika yote tunayofanya.

"Kujifunza Maandiko ya Biblia kutatusaidia kuishi kwa haki. Je! inawezaje kuwa hivyo?" Mwambie mwanafunzi mmoja asome Zaburi 119:9-11.

Sema: "Tunaweza kushinda majaribu ya Shetani kwa kutumia Neno la Mungu lililoko moyoni mwetu. Mtu ye yote aliye wa

na moyo wa kuwaongoza Israeli kumwabudu Mungu peke yake. Walicheza mbele za Bwana kwa nyimbo na kupiga tarumbeta walipoleta sanduku la Bwana katika mji wa Daudi.

Waisraeli walimtii Mungu, na Mungu alikuwa mwaminifu kwao. Aliwalinda na kuwabariki kwa kuwafanya washinde adui zao.

KULIFUNDISHA SOMO HILI

UTANGULIZI

Mwambie mwanafunzi mmoja asome Utangulizi kutoka kwa vitabu vyao.

Uliza: "Je! maisha ya Yakobo yaliwahusije Petro na Yusufu?" (Watapaswa kusema alionyesha maisha yaliyobadilika. Waliona kwamba yu tofauti sana nao.)

Uliza: "Je! tunaweza kujifunza nini kutoka kwake?" (Tunajifunza kwamba watu wengine wanapaswa kuona tukiwa tofauti katika maneno na matendo.)

Sema: "Watu walimwona Yakobo akiishi maisha aliyotangaza. Kujitoa kwake kwa Mungu kuliwavutia wale waliomwona. Alikuwa akifuata mfano wa Yesu."

MAELEZO

Sema: "Waisraeli walitaka kumrudia Mungu walipotambua kwamba wameacha kufuata njia zake. Walisahau kuwa waaminifi na kumwabudu Mungu pekee.

"Samweli wa Kwanza 7:3-4 inasema kwamba Samweli aliwaita watu wajitoe upya kwa Mungu. Walipaswa kuagana upya na Mungu. Aliwaambia waache kuabudu miungu na wamtumikie Bwana."

Uliza: "Je! watu walimrudia Mungu?" Soma kifungu cha 4.

na kuirithi nchi hiyo. Mungu alikuwa amewaahidi babu zao, lakini hasa walipaswa kuwa watiifu ndipo washinde.

Mungu alikuwa amewasaidia Waisraeli tangu watoke Misri. Aliwasaidia kujitayarishia vita. Aliwaambia silaha ya kutumia. Wao wangeshinda tu kama wangemwamini. Mungu aliwaleta '...amiri wa jeshi la Bwana.' (Yoshua 5:14) kwenda mbele yao."

Uliza: "Je! ni nani aliyewawezesha kushinda na kuirithi nchi hiyo?" (Alikuwa Bwana, kwa sababu walimtii.)

UKWELI KATIKA MAISHA YETU

Sema: "Waisraeli walishinda kwa sababu walimtii Mungu. Waliamini kwamba watashinda kwa nguvu za Mungu. Vita vyao juu ya Yeriko vilikuwa jaribu kuu la imani yao. Hawakwenda vitani kwa upanga na mikuki, lakini kwa kupiga tarumbeta na kelele.

"Wakristo wanaweza kushinda nguvu za Shetani kupitia kwa imani na utii katika Yesu Kristo. Wakristo humwelewa Mungu na Neno lake kupitia kwa imani. Imani huwawezesha kuelewa jinsi Mungu anavyofanya kazi maishani mwao. Hawaoni haya kumwita Mungu Baba yao kwa sababu ya Imani.

"Mungu ana mpango na maisha yako. Anataka utimize kwa imani na kumtii."

KUOMBA

1. Mwombe Mungu akuonyeshe mpango wake kwa maisha yako.

2. Mshukuru Mungu kwa ahadi alizotuahidi. Mwombe akusaidie wewe na wanafunzi wako kuzitimiza maishani mwenu.

3. Mwombe Mungu awasaidie wanafunzi wako kufuata mpango wake maishani mwao. Mwombe awasaidie wawe tayari kumtii na kumwamini.

SURA YA SABA

KUISHI KWA HAKI KANAANI

KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

SOMO KUTOKA: 1 Samweli 7

VIFUNGU VYA LEO: 1 Samweli 7

KIFUNGU CHA KUKUMBUKA: "...Wakasema, Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii" (Kutoka 24:7b).

KUSUDI LA SOMO HILI: Nitawafundisha wanafunzi wangu kwamba Mungu hutuza uaminifu wetu tunapomtii.

VITU VYA KUSAIDIA KUFUNDISHA: Hakuna

MSINGI WA SOMO HILI

Waisraeli walikuwa sasa katika Nchi ya Ahadi. Mungu aliwasaidia kushinda mataifa yaliyoishi katika nchi hii. Kanaani ilikuwa mali yao jinsi Mungu alivyoahidi. Wakanaani waliabudu miungu lakini Mungu alikuwa amewaamuru watoto wake, "Usiwe na miungu mingine ila mimi" (Kutoka 20:3). Lakini sasa walikuwa wanavutwa na miungu ya Wakanaani walianza kuacha njia za Mungu. Mungu ambaye ni Mungu wa wivu aliwafanya wateseke ili wamrudie.

Samweli wa Kwanza 2:1-2 inatambua jinsi Waisraeli walivyopata Sanduku la Bwana lililokuwa limechukuliwa na Wafilisti kwa muda wa miezi saba. Wafilisti walilichukua baada ya kuwashinda Waisraeli kwa vita. Waisraeli waliendela kumlilia Bwana hata ingawa walikuwa nalo kwa muda wa miaka ishirini. Maisha hayakuwa jinsi walivyotarajia.

Waisraeli walitamani kumheshimu Mungu kwa kuishi kwa haki. Walijua kwamba huo ndio mpango wa Mungu kwao. Alitaka Israeli wawe mfano kwa wengine. Walipaswa kumtii, kumwamini na kufuata mwongozo wake. Mataifa mengine yangemwona Mungu maishani mwao kama wangepanya mambo haya. Katika vifungu vya 3-4 Samweli aliwambia watu wajitoe upya kwa Mungu. Walipaswa kuagana upya na Mungu. Aliwambia Waisraeli wamwelekezee Mungu mioyo yao, na wamtumikie. Waisraeli walifanya hivyo! Walimrudia Bwana kwa mioyo yao yote, roho na nguvu zao zote.

Mungu alikuwa amemwita Musa kwenye Mlima Sinai na kumpatia amri za kuwaongoza Waisraeli. Walikumbushwa mara kwa mara kwamba Mungu anataka wamtii. Kufanikiwa kwao kama taifa kutategemea utu wa uaminifu wao kwa Mungu.

"Samweli akasema, Wakusanyeni Israeli wote Mispera, nami nitawaombea ninyi kwa Bwana" (1 Samweli 7:5). Watu waliitikia mwito wa Samweli walitambua dhambi zao na wakaomba msamaha. Walifunga na wakaitoa mioyo yao kwa Mungu. Samweli alikuwa tayari kuwaongoza watu kwa maombi ya kukiri na kumlilia Bwana. Alimtolca Bwana sadaka ya kuteketezwa, na akawaongoza watu kujitoe kumtii Bwana. Aliwasaidia kuwa na ushirika na Mungu.

Tunaona katika vifungu vya 8-10 kwamba Waisraeli walintegemea Bwana Mungu kuwakomboa. Walitambua kwamba ni yeye tu awezaye kuwakomboa. Jinsi walivyomlilia Samweli ilionyesha kwamba walikuwa tayari kumfuata na kumtii.

Katika 2 Samweli 6:5, 12-15 tunaona jinsi Daudi alivyowaongoza Waisraeli baadaye kumwabudu Mungu. Aliwaongoza nyumba ya Israeli katika nyimbo, kucheza vinubi na vinanda na kayamba. Soma kifungu cha 17. Daudi alikuwa